ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani

38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kwanza - Tarehe 14 Mei, 2014

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (*Pandu Ameir Kificho)* alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika mkutano wa kumi na sita mkutano ambao ni maalum kwa ajili ya shughuli za bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, karibuni sana na hongereni kwa kazi kubwa mliyoifanya huko nyuma na hadi kufikia leo tukawa tunakutana tena katika shughuli zetu kuanzia leo hii tarehe 14/5/2014.

Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya Spika ya leo inahusiana na kazi ambayo waheshimiwa Wajumbe mliifanya na ni lazima kwa mujibu wa taratibu zetu za kanuni kutoa taarifa kwenu. Kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe katika mkutano wa kumi na tatu wa Baraza la nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 9 Oktoba, 2013 hadi tarehe 22 Oktoba, 2013. Baraza lilipitisha miswada minne ya sheria ambayo ni kama ifuatavyo:-

1) Mswada wa Sheria ya kurekebisha sheria mbali mbali za ardhi na mambo yanayohisiana na hayo.
2) Mswada wa Sheria wa marekebisho ya usimamizi na utoaji leseni wa biashara na mambo yanayohusiana na hayo.
3) Mswada wa Sheria ya kufuta sheria ya biashara ya Zanzibar namba nne ya mwaka 1989 na kuanzishwa sheria ya biashara ya mwaka 2013 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
4) Mswada wa mwisho ulikuwa ni mswada wa Sheria ya kufuta na kuandika upya Sheria inayohusu kampuni na jumuiya nyengine kuweka masharti madhubuti zaidi ya uratibu na udhibiti wa kampuni Jumuiya na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe, kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha tisini kifungu kidogo cha tatu cha kanuni cha Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, naomba kutoa taarifa kwenu kwamba miswada hiyo sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais Wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio taarifa na hongereni kwa kazi hiyo nzuri ambayo mliifanya huko nyuma, ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kwa ruhusa yako naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutukutanisha tena na nikupongeze wewe na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kuanza vyema Baraza letu hili tukufu Mungu aliwezeshe kufanikisha shughuli zetu kwa salama na utulivu mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia Tarehe 23 Januari, 2014. naomba kuwasilisha.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/15. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam . 21

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Bismillahi rahmani rahim ama baada ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu alieniwezesha hapa kusimama na kuweza kuvuta pumzi zake ambazo ananiazima na sijui muda gani au dakika gani au saa ngapi atazihitaji. Huu si uwezo wangu wala maarifa yangu wala akili yangu ni neema kubwa ya Mwenyezi Mungu. Ni wangapi sasa hivi wanataka kusimama hawawezi wapo kwenye vitanda, wangapi wapo ICU sasa hivi wanasaidiwa pumzi.

Mhe. Spika, nitakuwa sijakutendea haki kama sikukushukuru wewe Mhe.Spika, na kukupa pole kwa kazi nzito uliyoifanya katika Bunge la katiba, kazi ambayo Bunge la katiba lile lilikuwa halina mzizi, halina anuani, halina *address*. Historia itajiandika kwa kazi uliyoifanya na Mheshimiwa Spika, nataka nikuulize leo umetolewa nyongo kwa kuwa mstahamilivu na msikivu kwa kazi nzito uliyoifanya.

Mheshimiwa, baada ya hayo leo hii tupo katika uwanja wa nyumbani baada ya kutoka katika uwanja wa ugenini, ninachoomba Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kama tuliyoyazungumza jana tujadili mambo yanayotuhusu, wananchi wanaangalia chombo chao cha wananchi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa kifo cha ndugu yake, baada ya hapo nataka nimshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais katika hilo suala ninalotaka kuliuliza la Na. 21. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jitihada zake za kuwa mstari wa mbele kuwafaraji wananchi waliopata mtihani huu. Mhe. Moh'd Aboud hili suala ni zito kwa wananchi wa Unguja Ukuu na maisha yao hivi sasa yapo hataraini naiomba Serikali ijibu suala hili kwa unyenyekevu wa hali ya juu.

Eneo la Unguja Ukuu kwa muda mrefu, limekuwa likitumiwa na Vikosi vya ulinzi kwa kufanya mazoezi ya kulenga shabaha. Harakati hizo zimeshasababisha madhara makubwa kwa wananchi wa Unguja Ukuu ambao wanaishi jirani na maeneo hayo au hutumia maeneo hayo kwa shughuli na mahangaiko ya kutafuta riziki**.**

Ni hivi karibuni tu kumeripotiwa tukio moja la wavuvi kuokota chuma ambacho kilileta mlipuko uliosababisha kifo kwa mmoja wao na wengine kujeruhiwa vibaya. Kuna taarifa pia kuwa matukio ya namna hiyo hutokea mara kwa mara ingawa mengine hayaripotiwi.

a) Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha haraka matumizi ya eneo hilo kwa mazoezi ya kulenga shabaha ili kunusuru athari za vifo na majeraha kwa wananchi wa Unguja Ukuu.
b) Serikali ipo tayari kulipa fidia kwa madhara yanayotokea na yatakayotokea kwa wananchi wa Unguja Ukuu walioathirika na watakaoathirika katika eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofiisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi Swali lake Nam. 21 lenye kifungu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelikabidhi sehemu ya eneo la Unguja Ukuu kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa ajili ya shughuli za mafunzo na ulengaji shabaha na kulipulia milipuko ya risasi isiyoliupuka wakati wa mazoezi.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali haina mpango wa kubadilisha matumizi ya eneo hilo lililokabidhishwa kwa JWTZ kwa matumizi mengine yoyote. Aidha, nichukue nafasi hii kuwasihi wananchi kutolitumia eneo hilo kwa shughuli zao za kijamii na kiuchumi ili kuepukana na madhara yatakayotokana na shughuli hizo za kijeshi kwani hakutokuwa na fidia itakayolipwa kutokana na madhara yatakayotokea.

Maana eneo hilo tayari limekabidhiwa kwa Jeshi kwa shughuli zao na kuna alama zinazoonesha kuwa eneo hilo ni la jeshi lisiloruhusiwa kwa shughuli za jamii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yasiyokuwa na afya ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza masuala mawili ya nyongeza.

Alipokuwa akijibu suala la msingi Mhe. Waziri alisema eneo lile wasilitumie wananchi kwa kiuchumi na mambo ya kijamii ambapo Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia eneo jengine mbadala baada ya pale, wakati eneo lile wanalitumia kwa mambo ya uchumi na kijamii.

La pili, sawa sawa na kuku na yai lipi limekuja mwanzo wananchi wa pale wamekuja mwanzo kabla ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, huoni kama ni dhulma wanayotaka kuifanya hivi sasa na kukiuka haki za binaadamu kwa kutowapa wananchi wale kutumia eneo hilo, unawaambiaje wananchi wa Unguja Ukuu hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamu wa pili wa Rais naomba kujibu suala la nyongeza lenye a na b la Mheshimiwa Jaku kama ifuatavyo;

Kama nilivyosema katika suala la msingi Serikali kwa sasa haina mpango wa kutafuta eneo lengine mbadala, kwa sababu tunapokwenda popote matokeo yake wananchi wanatufuata ni kwamba eneo lile tokea mwishoni mwa miaka ya 1960 Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume alikabidhi kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili litumike kwa ajili ya shughuli zetu za kiulinzi, cha msingi hapa ni kwamba wananchi wasitumie maeneo yale ambayo yana matatizo hayo kutokana na hali halisi ya shughuli za Jeshi.

Kama kuna tatizo lolote la wananchi la matumizi ya ardhi ni vizuri waonane na Mkuu wa Wilaya husika ili watengezewe eneo la kufanya shughuli zao za kijamii, lakini eneo lile kwa sasa haliwezi kutumika kwa shughuli nyengine zaidi ya shughuli za jeshi, na tuone umuhimu wa ulinzi wa nchi yetu. Mhe. Spika, pale ni eneo maalum limeshakuwa kuna hatari mbali mbali hususan mabomu kama alivyosema kwa hivyo sio maeneo ya kuchezea chezea na athari yake kupoteza maisha ya watu.

Kuhusu suala la pili Mheshimiwa wakati ambapo wanakabidhiwa jeshi eneo lilikuwa tupu ni baada ya jeshi kuwepo baadhi ya wananchi ndio wamehamia maeneo hayo. Cha msingi sasa tunaweza kushauri wizara husika ya ulinzi na kujenga taifa kuona umuhimu wa kulipa fidia kwa wale ambao wamo katika maeneo yale ili waweze kuhama na kuachia eneo hilo kwa jeshi na isiendelee kutokea matatizo makubwa ambayo yanaweza kutokea kwa kukaa karibu na kambi hiyo. Lakini kwa wale wapya watakaokwenda sasa hivi hakutokuwa na mazungumzo mengine yoyote isipokuwa kuondolewa katika eneo hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa waziri naomba kuuliza suala la nyongeza lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

a) Mheshimiwa Waziri nataka nikuulize kati ya wananchi na askari ni nani bora.
b) Kutokana na hali ilivyo hivi sasa, hivi wenzetu bara wana eneo *special* ambayo yapo nje na sehemu ya mbali kabisa wanafanya mazoezi hayo bila ya tatizo lolote.

Mheshimiwa Waziri huoni sasa hivi ipo haja ya kuwa eneo hili ni dogo la Zanzibar na kutokana na tatizo la wananchi wasiendelee kwa kuathirika na mabomu, huoni ipo haja Mheshimiwa ya kwenda kuombwa eneo la kufanyia mazoezi la majeshi kule Tanzania Bara.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa Serikali yoyote ulimwenguni inaheshimu sana wananchi wake na hawa wananchi baadhi yao ndio askari wetu, na askari wetu wapo pale kwa ajili ya kuwalinda wananchi hao hao ndio maana tukawa na askari kwa kuwapenda wananchi wetu. Si kwamba hatuwapendi wananchi wetu maana ya kuwa na akari ni kwa sababu ya kuwa na mapenzi makubwa na wananchi wetu ili wawalinde wananchi hao wasipate matatizo.

Unapoondoa askari maana yake ni kuvamiwa katika nchi yako na ujue sote hapa tutakuwa hatupo, kwa hivyo umuhimu wa kuwa na askari una umuhimu wake na mapenzi yetu kwa wananchi utaendelea kuwepo na hatuwezi

kurudi nyuma. Serikali kuendelea kupenda wananchi wake na moja katika kupenda ni kuwawekea askari ili wawalinde.

Mheshimiwa hakuna askari yoyote yule asiyehitaji eneo la mazoezi huwezi kusema tuwatoe askari hapa wakafanye mazoezi bara, lazima wafanye mazoezi katika eneo hili ili litakapotokea tatizo lolote la kuvamiwa ama tatizo lingine ili askari wajenge uelewa mzuri katika maeneo haya ya kuwalinda wananchi na nchi yao, ili tuendelee kuwa katika hali ya salama na amani.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana leo hapa kwa mintaarafu ya kupanga mambo yetu ya kitaifa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba Jeshi ni kitu muhimu katika nchi hii. Lakini pia serikali yoyote ile huweza kupanga taratibu zake kwa mintaarafu ya kuona kwamba nchi hii inahitaji sehemu fulani na fulani na fulani kuweka wanajeshi wake. Je, anaelewa kwamba sehemu ile tokea 1964 palikuwa pori tupu hata huyo mwananchi alikuwa hajahamia pale, atakubaliana nami hivyo. Ni vyema sisi watunga sheria humu ndani Mhe. Spika, tukakubaliana na eneo lile kwamba bado liendelee na mambo yanayohusiana na jeshi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru na niseme nakubaliana nae kwa asilimia 100 na ni kweli eneo lile lilipewa jeshi muda mwingi uliopita kama nilivyosema tokea mwishoni mwa miaka ya 1960 na marehemu Mzee wetu Abeid Aman Karume, kwa nia njema ya kulinda nchi yetu na wananchi wake.

Kwa hivyo ni imani ya serikali kwamba jeshi litapewa nafasi lifanye wajibu wake na wananchi waheshimu sana maeneo yale, kwa sababu yanaweza kuhatarisha maisha yao kwa kuingilia katika maeneo hayo. Sote tumeona kilichotokea Gongo la Mboto - Ukonga Dar es Salaam, tuombe Mungu mambo kama yale yasitokee kwenye nchi yetu.

Kwa hivyo si vizuri hata kidogo kwa wananchi kuingia katika maeneo yale ambayo ni hatari yanaweza kusababisha athari kubwa ya maisha yao. Ninachosema kwa wale wananchi ambao wamejenga sasa ndani ya maeneo ya jeshi, tutawasiliana na wizara husika ili tuweze kutengeneza fidia kwa wale waliomo na waweze kuhama maeneo hayo kwa sababu yanahatarisha maisha yao na tuwaombe wananchi wasende katika maeneo yao. Na la msingi ni kuonana na Mkuu wa Wilaya husika ili wapate maeneo mengine ya shughuli zao za kilimo na nyengine za kimaisha. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 77

Hatua Kwa Kampuni Zinazoajiri Wageni Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na wageni wanaoingia nchini kutoka nchi mbali mbali kama vile Tanganyika na Kenya nk, na kupatiwa ajira kwenye mahoteli na makampuni ya watu binafsi hapa Zanzibar.

Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya makampuni yanayoajiri wageni na kuacha vijana wetu wengi kukosa ajira.
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mwakilishi suala lake napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira nambari 11 ya 2005 wananchi wanaoingia kutoka Tanzania Bara, hawachukuliwi kama ni wageni na kwa hivyo, wanapata fursa za ajira kama ilivyo kwa wananchi wa Zanzibar wanaoingia Tanzania Bara. Kwa vile wananchi wa Zanzibar na wao hufaidika na fursa mbali mbali za ajira ziliopo Tanzania Bara ilimradi wanazo sifa na uwezo wa kufanya kazi husika. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 77 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Zanzibar imekua ikichukua hatua mbali mbali katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata fursa za ajira kupitia Makampuni binafsi hapa Zanzibar. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kukaa pamoja na waajiri na kuwahimiza kutoa vipaumbele zaidi vya ajira kwa vijana wetu ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio ya hatua hizo ni kwamba, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya vijana 340 (wanaume 252 na wanawake 88) walipata fursa za ajira kupitia Makampuni binafsi mbali mbali ikiwemo sekta za mahoteli.

Aidha, kupitia Kampuni binafsi ya DANAOS, jumla ya vijana wa kiume 410 wa Zanzibar walipata fursa ya ajira za ubaharia. Vijana 13 (wanaume 11 na wanawake 2) wameajiriwa kupitia kampuni binafsi za simu za mkononi. Idadi hii ni kwa vijana waliojiorodhesha kupitia Idara ya ajira pekee.

Vile vile Serikali kupitia Wizara yangu inaendelea na hatua za kuwataka vijana wabadili mitazamo yao ya kupenda na kutokuchagua kazi ili iwe rahisi kupata fursa hizo za ajira kupitia Makampuni hayo binafsi.

Mhe. Spika, mafanikio hayo yote yanatokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali za kukaa pamoja na watendaji na viongozi wa Makampuni Binafsi na kujadiliana njia bora zaidi za kukuza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kutumia kanuni yako ya Baraza la Wawakilishi, kifungu namba 37 Waziri au mjumbe yoyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi isipokuwa kwamba swali alilouliza Waziri moja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine na Mwanasheria Mkuu.

Swali langu Mhe. Spika, niliuliza, je serikali inachukua hatua gani dhidi ya makampuni yanayoajiri wageni na kuacha vijana wetu wengi kukosa ajira. Jawabu serikali ilikuwa inijibu, yapo makampuni hayo au hayapo hivi sivyo nilivyouliza swali langu Mhe. Spika, naomba swali lirudi tena likapangiwe na wajumbe nisaidieni kwa suala hili ndivyo nilivyouliza na jawabu nililopewa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma): Mhe. Spika, swali ambalo limeletwa ofisini kwangu kwa idhini yako naomba kutoa ufafanuzi. Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na wageni wanaoingia nchini kutoka nchi mbali mbali kama vile Tanganyika, kwanza nataka niseme nchi mbali mbali Tanganyika si nchi ya kigeni. Tanganyika ilikuwa nchi ya kigeni kabla ya 1964, lakini baada ya 1964 Tanganyika iliungana na Zanzibar. Kwa hivyo Kenya na kadhalika kupatiwa ajira kwenye mahoteli na makampuni ya watu binafsi hapa Zanzibar. Je, serikali inachukua hatua gani dhidi ya makampuni yanayoajiri wageni na kuacha vijana wetu kukosa ajira.

Mhe. Spika, suala alilouliza Mhe. Jaku nimelijibu kwa mujibu wa taratibu za shughuli za Idara yangu inavyofanya kazi. Akitaka nimjibu anavyotaka yeye nadhani hiyo sio sawa. Kwa hivyo swali nimelijibu na kama ana swali la nyongeza aulize mimi nipo nitamjibu, kama hana akae kitako awaachie waheshimiwa wengine waulize swali. *(Makofi).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Waziri au Mjumbe yoyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu na kwa usahihi, kwa ufupi isipokuwa kwamba swali alilouliza Waziri mmoja linaweza kujibiwa. Swali langu Mhe. Spika, hebu nisaidieni, serikali inachukua hatua gani dhidi ya makampuni yanayoajiri wageni, Waziri anijibu zipo au hazipo, kwisha. Lakini nakuja kuulizwa jibu jengine hakuna. Mimi anijibu Mhe. Waziri bila ya ubishano wowote, makampuni yapo yanayofanya hivi au hayapo basi ndio suala nililoulizwa Mhe. Spika. Nimeandika kiswahili wala sijaandika kihindi Mheshimiwa Spika, humu ndani.

Mhe. Spika: Anachouliza Mhe. Jaku sasa tusikilizane waheshimiwa wajumbe je, kuna makampuni ambayo yanaajiri wageni. Kama hayapo sawa kama yapo unaweza ukaeleza kama unazo taarifa Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma) Mhe. Spika, alianza na kuzungumzia utataribu wa kujibu swali na mimi nilianza kujibu swali kwa swali alilouliza la utaratibu wa kujibu swali na ndio maana nikamwambia kama ana

swali la nyongeza angeuliza. Sasa hili ni swali la nyongeza, ilikuwa halina haja na utangulizi ambao ameuanza. Utangulizi ambao ameuanza kama kwamba hili jibu nililojibu ni *wrong*. Mimi ninajihisi serikali imejibu swali sahihi. *(Makofi).*

Sasa kama swali lake la nyongeza ni kwamba yapo makampuni ya kigeni au hayapo, yapo na ndio maana nimemalizia kwa kusema Ofisi yangu inakaa na makampuni husika na waajiri kukaa nao na kuzungumza nao kuhusu utaratibu wa ajira binafsi katika nchi yetu. Mwisho wa swali langu nimesema hivyo.

Kwa hivyo kama anataka nimjibu ndio au hayapo, yapo makampuni na ndio maana serikali imesema hivyo. Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri katika maelezo yake alisema kwamba wako vijana ambao wameajiriwa kutoka Tanzania Bara hapa Zanzibar na wapo vijana ambao Zanzibar kwenda Tanzania Bara pia wameajiriwa. Je, Mhe. Waziri nikuulize vijana wangapi wa Zanzibar ambao wameajiriwa Tanzania Bara na vijana wangapi wa Tanzania Bara ambao wameajiriwa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma) Mhe. Spika, swali lake linahusu takwimu naomba swali hilo, kwa sababu linahusu takwimu za walioajiriwa Tanzania Bara na walioajiriwa Zanzibar nimletee kwa njia ya maandishi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii nikamuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri kama hivi ifuatavyo; Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri alivyoweza kutoa ufafanuzi hasa kwa vijana ambao waliajiriwa kwa upande wa Tanzania Bara lakini vile vile Zanzibar. Swali langu liko hapa. Mhe. Spika, kwa kuwa malalamiko ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika makampuni binafsi wameyaleta mpaka kwenye kamati zetu husika za Baraza na wanalalamika kwamba ajira ambazo wanazopewa wageni ambazo nyingi zao wazawa, wazalendo wanaziweza lakini bado yale yanaendelea kun'gan'gania kuajiri wafanyakazi kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, swali langu liko hapa.

Je, Mhe. Waziri huoni kwamba sasa hivi wakati umefika kwa yale makampuni ambayo yameajiri wafanyakazi ambao wanatoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na katika nafasi zile wazalendo wanazo haoni Mheshimiwa iko haja sasa hivi kuwafutia vibali vyao vya kazi na kuwarejesha makwao. Lakini vile vile Mhe. Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni katika maadhimisho ya miaka 50 wakati wa maandalizi kuna wafanyakazi vile vile hasa katika kitengo cha Afya kama sikosei walilalamika sana kwamba kuna baadhi ya taasisi mbali mbali Tanzania Bara, ambao na wao wameajiri wafanyakazi kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao nafasi zile zilikuwa na uwezo wa kuchukuliwa na wazawa. Na Mhe. Rais alitoa agizo kwamba wale wafanyakazi ambao wa nje wanafanyakazi Tanzania ambao nafasi zile wazalendo wanaziweza wafutiwe vibali mara moja.

Sasa kwa kuwa na sisi tuko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haoni Mheshimiwa Waziri kwamba aweze kutekeleza agizo ambalo alilolitoa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wahakikishe kwamba ajira kwanza zinaanza kwa watanzania halafu baadae kwa zile nafasi ambazo hawana uwezo nazo ndio zije kwa wageni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma) Mhe. Spika, kuhusu suala la malalamiko ya vijana wetu kwa ajira wanazopewa wageni nadhani hili tayari serikali ilishachukua hatua ya kukaa na waajiri binafsi na makampuni ya sekta binafsi na kuwaeleza taratibu na sheria ya kazi na ajira inayoeleza hapa Zanzibar. Na ndio maana tuna makubalino ya kukaa pamoja na makampuni haya kuweza kuona kwamba zile nafasi ambazo wazanzibari au wenyeji au watanzania wanazo basi ni vizuri wakaajiriwa. Na zile ambazo utaalamu huo haupo basi wakatafuta wataalam kutoka nje.

Sasa suali la kufuta vibali vyao, bila shaka kwa sababu sheria za kazi zipo na sheria za ajira zinaeleza wazi pale ambapo muekezaji yeyote au mmiliki wa kampuni yeyote akivuka masharti basi bila shaka Kamisheni ya Kazi kupitia Idara hii ya Ajira wataweza kufuta kibali cha muekezaji ambaye anavunja masharti ya sheria za nchi yetu.

Suala la kufuata agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nadhani kama agizo hilo lina uwezo wa kuingia mpaka Zanzibar kuhusu zile sekta zinazoidhinishwa kwa mujibu wa sheria ya muungano inabidi lazima na sisi tutekeleze agizo hilo. Lakini kama agizo lile lilikuwa linahusu sheria zinazohusu uwekezaji wa Tanzania Bara kwa maana Serikali ya Jamhuri ya Muungano, zile sheria ambazo hazifanyi kazi hapa Zanzibar hilo basi tutakuwa vigumu sisi Zanzibar kuweza kulifata. Lakini kama sheria hizo zinaruhusu zifanye kazi Zanzibar basi tutaweza kuzitekeleza bila ya matatizo yoyote yale.

Nam. 43

Kupoteza Hadhi kwa Mchezo wa Mpira wa Miguu Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Mpira wa miguu mbali na kutoa Burudani kwa wananchi walio wengi nchini sambamba na kukonga nyonyo za wazanzibari wengi, umekuwa ni chaguo la wazanzibari wengi katika rika tofauti. Kwa bahati mbaya wapenzi wengi wa mchezo huo wamevunjika moyo kutokana na timu zetu za Zanzibar kufanya vibaya siku hadi siku, jambo lililopelekea mchezo huo kupoteza hadhi hapa nchini.

Je, tatizo ni kutokana na timu zetu kukosa uwezo wa kufanya usajili ulio makini au mamlaka husika (ZFA) kutokuwa makini katika kusimamia soka letu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 43 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalosababisha timu zetu kutofanya vizuri ni migogoro ya siku nyingi iliyotokea kwenye chama cha michezo. Lakini hivi sasa Mhe. Spika, tatizo hilo limeondoka na sasa hivi Wizara yangu kwa kweli inafuatilia vya kutosha kuhusu migogoro ya ZFA.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Samahani Mhe. Spika, kwa kusimama bila ya amri yako. Kwanza naomba radhi. Baada kuomba radhi naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema chanzo cha matatizo ya soka katika nchi yetu, mchezo unaopendwa sana katika nchi hii wakiwemo wapiga kura wangu wa Jimbo la Wawi, wapiga kura wa Jimbo la Nungwi na Tumbatu pia wanapenda soka hili. Kwa sababu umekiri kwamba tatizo ilikuwa ni mgogoro uliokuwepo kwa muda mrefu katika *ZFA*, na kwa kuwa viongozi mliyopo Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Waziri mlikuwa mpo na mgogoro ule ukawa unavukuta tu mpaka kuiteremshia hadhi soka yetu.

a) Je, kwakufanya hivyo nikushindwa kuwa makini katika kazi zenu au hamna uwezo wakuongoza hiyo Wizara.
b) Mheshimiwa mimi nadhani chanzo kikubwa cha tatizo la soka katika nchi yetu nikushindwa kuitumia hazina zilizopo kwa maana ya makocha wa ndani ya nchi, hasa kwa vile hatuna uwezo wakuajiri makocha kutoka nje.
   Je, ni lini wizara hii inayoshughulika na mambo ya soka itatoa faraja kwetu sisi kwa kutuajiria vijana wazuri katika ukocha akiwemo kijana wetu Suleiman Mahamoud Jabiri ambaye amewatoa watoto wa mitaani na wakachukua kombe la dunia, sisi tunashindwa kumtumia hapa?
c) Kuna hazina zinatoka Zanzibar pale Marmul kwa mfano Thuweni Ali yupo Marmul Oman, yupo Abdul Wakati Juma, yupo Lhamy amekaa na anafundisha timu pale pale Oman. Ni lini mtatoa vijana wetu wale kina Abdul Wakati Juma, Thuweni Ali, Inocent Haule na kuwaleta hapa kuja kufundisha soka hili nakuweza kuinua soka kama walivyoinua pale Oman. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Saleh tangu kipindi nilipoteuliwa mimi Naibu Waziri swali hili analiuliza kila siku, kila tukija kwenye kikao Mheshimiwa tunatoa ufafanuzi wakutosha na tunaeleza kwa kina, sasa nashangaa Mhe. Saleh ikiwa swali hili kila leo analirudisha. Kwa sababu nataka nikwambie Mhe. Saleh kitu chochote kile kila siku ukikila huwa hakina hamu yoyote. Sasa nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili, hiyo ni misamiati ya Kiswahili Mhe. Spika…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe…

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Hiyo ni misamiati ya Kiswahili sasa kama wao wamefikiria vyingine ni wao, lakini…

Mhe. Spika: Hebu tumsikilize Mhe. Naibu Waziri…

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Lakini ni misamiati ya Kiswahili na lahaja za Kizanzibari.

Mhe. Saleh mimi najua nimejibu swali hapa kwa faida ya wananchi, lakini ilikuwa Mhe. Spika, swali hili nikwambie kuwa swali hili kila mara tunalirejea kila kipindi cha kikao cha Baraza, si kikao cha kawaida wala si kikao cha bajeti, lakini nimejibu kwa faida ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania nzima.

Sasa nawahakikishia Wajumbe nawaomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wizara yangu inatekeleza majukumu yake na inafuatilia shughuli zake kama kawaida siku hadi siku. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi maswali yakishajibiwa isiwe ni kila siku swali hilo na matatizo yaliyokuwepo tumeeleza kuwa *ZFA* ilikuwa na matatizo Rais aliyepita na sasa hivi huyu Rais aliyepo anafuatilia majukumu yake kama kawaida. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Saleh nataka nimwambie hivyo.

Mhe. Spika: Hebu kuhusu utaratibu, unasemaje Mhe. Saleh?

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, hili ni Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Mabunge ya *Commonwealth* na yana kanuni kama yalivyo Mabunge mengine ya *Commonwealth*, mtu anatakiwa awe na uhakika anachokisema katika aidha anapokuwepo huku *back bencher* au anapokuwa hapo mbele …

Mhe. Spika: Mheshimiwa kuhusu utaratibu chini ya kanuni ipi?

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nasema kwamba hili swali haliulizwi kila siku hana uhakika kwamba linaulizwa kila siku, na kama ingelikuwa linaulizwa kila siku ofisi yetu hii ya watendaji hapa ina wataalamu wengi tu wa sheria na mambo ya *political science* wasingelileta katika Baraza. Ni kwamba hili swali halijapita, kwa hivyo hana uhakika na afute maneno hayo na anijibu maswali yangu yote (a), (b) na (c).

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Nina maelezo Mheshimiwa, Mhe. Spika, kwa kweli haya ninayoyasema yote yana uhakika kwa sababu hili swali amebadilisha tu lakini ni swali lile lile la kawaida analoliuliza. Mimi nina uhakika yote ninayoyasema kwa sababu najibu maswali mimi hapa nisingesema hivyo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi yakuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpe hongera Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali kijasiri. Mheshimiwa hivi karibuni *league* yetu ya mpira wa miguu Zanzibar *(premier league)* ya Zanzibar ilimalizika nakupata washindi wawili ambao watawakilisha katika mashindano mbali mbali ya Afrika.

Je, Wizara, Baraza la Michezo na *ZFA* yenyewe imejipanga vipi kuzisaidia vilabu hivi ili kujiandaa na mashindano haya isiwe kila mwaka tunashiriki tu, twende tushindane na tushinde na kuiletea sifa Zanzibar kwa ushindi wakusonga mbele katika mashindano mbalimbali ya Afrika. Je, wizara imejipanga vipi kuwasaidia timu zetu hizi ambazo zinashiriki katika mashindano mbalimbali ya Afrika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa namna ambavyo alijibu swali mama kuhusiana na swali la nyongeza la Mhe. Nassor Salim Ali (Al-Jazira) ni kwamba wizara kwanza inazipongeza timu ambazo zimepata ushindi mwaka huu na kwamba tutajitahidi kwa kadri yetu na uwezo wetu kushirikiana na uongozi wa klabu zenyewe kufanya maandalizi ya awali. Lakini pia wakati ukifika kuwasaidia kwenda katika mashindano haya sisi wizara kupitia Baraza la Michezo kuwasaidia gharama za kusafirisha kwenda katika michezo inayohusika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nilikuwa naomba nimwambie kwamba ukiona watu wanauliza sana maana yake majibu yako yalikuwa siyo. Swali langu ni kwamba kwa kuwa umekiri kwamba *ZFA* muda mrefu ilikuwa ikiendeshwa kwa migogoro. Je, wananchi wasikitike kwamba fedha yao ya Baraza la Wawakilishi iliyokuwa ikiidhinishwa ilikuwa iko pale kwa ajili ya migogoro badala ya kazi ya mpira.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza ni kweli kwamba kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwa muda mrefu Chama cha Mpira wa Miguu *(ZFA)* Zanzibar kilikuwa na migogoro mikubwa, na jitihada zimefanyika sana kuhakikisha kwamba migogoro hiyo imemaliza. Lakini naomba nimfahamishe mjumbe kwamba kwa kiwango kikubwa *ZFA* inajiendesha kwa fedha zake wenyewe, sisi kama Serikali na kupitia Baraza la Wawakilishi fedha ambayo inaidhinishwa hapa ni fedha ndogo sana ambayo inatumika kuwapa ruzuku kama vyama vyingine.

Sasa fedha hiyo haijatumika katika kuhimiza migogoro, wala fedha hiyo haijatumika katika kutatua migogoro. Fedha hiyo kwa kiasi fulani imesaidia katika angalau kupata fedha kwa ajili yakusaidia masuala ya undeshaji pale ambapo *ZFA* imeshindwa. Lakini kwa ufupi kwamba fedha nyingi ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, ni ruzuku ambayo imekuwa ikigawanywa kwa vyama 30 vilivyosajiliwa ikiwemo *ZFA*. Kwa hiyo, mgao mdogo sana huo wanaopata *ZFA* unatumika zaidi katika suala la uendeshaji na siyo katika kutatua migogoro ambayo iliikumba *ZFA.*

Nam. 88

Kupanda kwa bei ya Bidhaa za Chakula

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa hivi sasa bei za bidhaa za chakula zimepanda sana na kusababisha maisha ya Wazanzibari kuwa magumu.

a) Je, Serikali ipo tayari kuwaeleza wananchi nini chanzo cha upandaji wa bei hizo.
b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali katika kupunguza makali ya maisha yaliyosababishwa na hali hiyo.
c) Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa wananchi ili nao kwa upande wake washiriki katika kushusha bei za vyakula ndani ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake Nam. 88 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mwenendo wa bei za chakula muhimu kama vile mchele, sukari na unga wa ngano umeendelea kuwa wa utulivu kwa kipindi kirefu kutoka na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuendelea na hatua za kusimamia bei hizo, na pia hatua za kisera zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zakushauriana na wafanyabiashara wa bidhaa hizo na kukubaliana kwa pamoja juu ya bei za uuzaji wa reja reja wa bidhaa hizo.
Kwa kipindi kirefu sasa bei za reja reja za mchele Mhe. Spika, ni wastani wa 1000-1100/=…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hebu niombe utulivu tusikilize majibu ya swali liloulizwa…

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Sukari shilingi 1300-1400/= kwa kilo na unga wa ngano ni shilingi 1100/= kwa kilo.

Mhe. Spika, kwa upande wa bidhaa nyengine za chakula hasa za tungule, vitunguu, mbatata, tangawizi na bidhaa nyenginezo za mboga mboga kumejitokeza ongezeko la bei hasa kwa kipindi cha January-Mach 2014. Ongezeko hilo Mhe. Spika, linatokana na uzalishaji mdogo wa ndani ya Zanzibar pamoja uzalishaji mdogo kutoka Tanzania

Bara uliosababishwa na kuwepo kwa hali mbaya ya hewa, hivyo kuwepo ugumu wa upatikanaji wa bidhaa za aina hiyo. Mabadiliko ya hali ya hewa Mhe. Spika, yaliathiri usafiri na usafirishaji wa bidhaa hizo kwa njia ya bahari.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko inawaomba basi wananchi kuelekeza nguvu zao zaidi katika kilimo hasa cha bidhaa za aina hizi kwa kuwa hazihitajia eneo kubwa la ardhi katika kilimo chake. Na pia soko la bidhaa hizo lipo lakutosha kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

a) Je, pamoja na bei hizo Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wakuzishusha bei hizo kwa vile wananchi wetu uwezo wao ni mdogo.
b) Je, Serikali ina mpango wa muda mfupi wakushusha bei hizi hasa ukizingatia mwezi huu mtukufu wa Ramadhani kwa dharura ili kuwapunguzia makali wananchi wetu wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, nimesema wakati nikijibu swali la msingi kwamba tunawaomba wananchi waongeze nguvu katika uzalishaji wa mazao hayo ya mboga mboga na bidhaa ambazo tunaziagiza kutoka Tanzania Bara. Kwa sababu kimsingi Mhe. Spika, mazao haya uagizishiaji wake kutoka Tanzania Bara huwa hauratibiwi na wizara yetu zaidi yakuweka takwimu za idadi yakuingiza pamoja na kuangalia bei, lakini kuratibu bei siyo rahisi kwa sababu inategemea zaidi hali ya hewa na uingizwaji wa bidhaa hizo kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi ongezeko la bidhaa kila leo, kila kesho linaongezeka na wenye vyombo ambavyo wanaobeba mizigo kuleta huku.
b) Mhe. Naibu Waziri hivi sasa Serikali ingekaa zaidi ikaangalia ushushaji wa kodi za bidhaa ili zaidi wananchi waweze kunufaika na hasa kutokana na mishahara yenyewe ni midogo wanaopewa wafanyakazi. Mhe. Naibu Waziri hili suala naomba sana ili uliweke kwenye bajeti hii, umuombe Mhe. Waziri wa Fedha aweze kuwasaidia wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, hatuna uhakika wizara juu ya ongezeko la bei ya usafirishaji wa bidhaa hizo kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar, lakini nilimwambia kwamba atalifuatilia hilo ili kupata uhakika kama limechangia katika upandishaji wa bei ya bidhaa hizo kutoka Tanzania Bara.

Hata hivyo nimjibu suala lake la pili Mhe. Makame Mshimba kwamba suala la mshahara mdogo ni suala ambalo linaangaliwa na Serikali na awe na subra, tusibiri bajeti itakayosomwa jioni hii na Waziri wa Fedha tuone Serikali itakabiliana vipi na suala hilo.

Mhe. Thubeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kama upandaji wa vyakula bei kama mchele, sukari, unga wa ngano na bidhaa nyingine ambazo huletwa kutoka nje zinaongezeka kutokana na ongezeko la bei duniani, na ikiongezeka bei basi inabidi na vyakula hupanda.

Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kama sisi wananchi wa Zanzibar tunafaidika na kuongezeka bei tu hatujawahi kushuka kwa bei, ikipanda bei duniani tunapanda nayo, ikishuka bei duniani na sisi tukashika. Lakini sisi bei inapanda na ikishapanda na ikishafika ndiyo imefika hairudi tena.

Ni lini Serikali itafuatilia na kuona kama ikipanda bei duniani tunapanda nayo na ikishuka tunashuka nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nikubaliane nae kwamba kwa kiasi kikubwa bei za mchele, sukari na unga zinategemea bei ya soko la dunia, lakini kama amenisikiliza vizuri Mhe. Mwakilishi wakati nikijibu swali la msingi, nimesema kwamba ni muda mrefu sasa kwa kipindi hiki kuanzia

Januari-Mach bei za bidhaa hizo sukari, mchele na unga wa ngano zimekuwa zikienda katika wastani mzuri sana haijaongezeka, na hali hii inatokana na kwamba tumejenga utaratibu mzuri wa Serikali kupitia wizara kukaa na wafanyabiashara ili kutathmini kwa pamoja nakuweka bei na tunakubaliana kwa pamoja.

Kwa hiyo, kwa kipindi kirefu sasa mazao hayo hayajapanda bei, kilichopanda bei ni hizi bidhaa za mazao ya mboga mboga kama nilivyosema kwenye jibu langu. Hizi zimetokana na kuharibika kwa hali ya hewa Tanzania Bara ndio maana bei hizo sasa zinakuwa zinapanda.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri na sasa tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2014/2015

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kabla sijawasilisha Hotuba yangu nina ombi maalum kwa Waheshimiwa Wajumbe; ombi lenyewe Mhe. Spika, pamoja na nakala za hotuba yangu zilizowasilishwa mapema asubuhi, pia tumepata vitabu viwili. Kitabu cha kwanza kinaonesha Mapitio ya Hali ya Uchumi mwaka 2013 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar kwa mwaka 2013/2014. Kitabu cha pili, Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo Zanzibar wa mwaka 2014/2015.

Sasa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na hotuba yangu, lakini hivi vitabu viwili viwe pia ni hadidu rejea zetu. Mimi nitawasilisha *summary* lakini mambo yote yameelezwa kwa kina katika vitabu viwili hivi. Naomba sana Waheshimiwa tuvitizame kwa undani zaidi hivi vitabu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ili liweze kupokea, kujadili, na hatimae kuidhinisha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2014/2015. Taarifa hizi ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II), Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa MKUZA II na Ilani ya CCM ya mwaka 2010/2015.

Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/14 na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya, uzima na kuweza kukutana tena hii leo katika Kikao cha Bajeti kujadili Hali ya Uchumi kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kikao hiki kuendesha kazi zake kwa amani, usalama, utulivu na upendo kati yetu ili tuweze kukamilisha vyema malengo yetu tuliyokusudia.

Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake makini, hekima na utulivu wake katika kuiongoza Zanzibar yetu. naomba pia kumshukuru kwa maelekezo yake ambayo yametuwezesha kuwasilisha taarifa hii ya hali ya uchumi kwa mwaka wa 2013 na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Ni dhahiri uongozi huu mzuri wa Mhe. Rais umewashirikisha wasaidizi wake wakuu, Mhe. Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais. Naomba niwapongeze kwa dhati na kuwashukuru kwa uongozi wao thabiti.

Aidha, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Tume ya Mipango kwa miongozo yao wanayotupatia katika ukusanyaji na usimamizi wa mipango ya maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Baraza hili na pia kunipatia fursa ya kuwasilisha taarifa hizi. Vile vile, nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura ambae ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kutupatia maoni na ushauri ambao umesaidia kuimarisha taarifa hizi ninazowasilisha hivi leo.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendelea kuipatia kamati ushirikiano mzuri katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, shukurani pia ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mchango wao katika maandalizi ya taarifa hii, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inathamini sana michango yao waliyoitoa.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa mashirikiano yao waliyonipatia wakati wa maandalizi ya taarifa na hotuba hii. Aidha, nawashukuru Ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Ndugu Amina Khamis Shaaban, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango. Vile vile naomba kuwashukuru Wakuu wa Idara na Wafanyakazi wote wa Taasisi hizi mbili kwa kufanikisha utayarishaji wa hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa kuchaguliwa kwa wingi wa kura kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiembe Samaki kwa tiketi ya CCM. Ni matumaini yetu kuwa ataitumia vyema imani aliyopewa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wake na wananchi wa Kiembe Samaki kuwa Mwakilishi wao kupeleka mbele gurudumu la maendeleo katika Jimbo hilo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 unaotarajiwa kumalizika hivi karibuni, nchi yetu imepata faraja ya kusherehekea kwa mafanikio, sherehe adhimu ya kufikia miaka 50 ya Mapinduzi yetu Matukufu ambapo wananchi wetu waliondokana na Madhila ya Ukoloni. Aidha, tumeweza kusherehekea miaka 50 ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindiuzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kuwemo katika Marais waliotufikisha katika sherehe hizi. Aidha, naomba kuwapongeza wananchi wote wa Tanzania kwa kuadhimisha sherehe hizi kwa salama, amani na utulivu.

Mhe. Spika, wakati tunaadhimisha sherehe hizi za miaka 50 nchi yetu imo katika kuandika historia nyengine ya kuandika Katiba mpya, ambayo tunaamini itapofanywa vizuri itatuchukua zaidi ya miaka 50 mingine ijayo. Hivyo, nawaomba Wahehsimiwa Wabunge wenzangu wote wa Bunge Maalum la Katiba kutumia fursa hii adhimu kutoa Katiba bora itakayozingatia maslahi ya wananchi. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe subira na uvumilivu katika mchakato huo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuendelea kuimarisha uchumi na kuwapunguzia umasikini wananchi wake katika kukuza Sekta ya Utalii na kuipeleka katika hatua nyengine ili kuleta tija zaidi kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Katika kufikia lengo hilo, serikali iliandaa maabara ya utalii, mazingira bora ya biashara na utafutaji wa Rasilimali Fedha iliyobeba ujumbe wa Matokeo kwa Kuimarisha Ustawi, (*Results for Prosperity - R4P)* ambapo wadau kutoka Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Wasomi na Asasi za Kiraia walishiriki. Maabara hayo yaliibua programu tatu za kuendeleza Utalii, Biashara na Rasilimali Fedha ambazo zilitekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2014 - 2015.

Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo serikali imetayarisha vipaumbele vya utafiti kwa Zanzibar kwa dhana ya tafiti na maendeleo, vipaumbele hivi vya utafiti vinalenga kuisaidia Zanzibar kutimiza malengo yake ya Dira ya Maendeleo ya 2020 na MKUZA, ambapo matarajio ya Zanzibar ni kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2020.

Mhe. Spika, hotuba ninayowasilisha leo imegawika katika sehemu kuu tano; kwanza ni Mapitio ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2013, pili ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2013/14, tatu ni Mwelekeo wa Hali ya Uchumi mwaka 2014, nne ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/15 ikiwemo Rasilimali Fedha na mwisho ni Hitimisho.

MAPITO YA HALI YA UCHUMI

Hali ya Uchumi Duniani

Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Spika, uchumi wa dunia umefikia ukuaji wa wastani asilimia 3 mwaka 2013 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2012. Uchumi wa nchi zilizoendelea umefikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2013, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2012. Uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi umefikia wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2013 kutoka wastani wa asilimia 5 mwaka 2012. Kasi hii ndogo ya ukuaji wa uchumi inatokana na kuendelea kudorora kwa uchumi katika nchi za Ulaya, udhibiti wa ukomo wa matumizi ya bajeti, mabadiliko ya hali ya hewa, machafuko ya kisiasa mashariki ya kati na baadhi ya maeneo ya Afrika kama vile Congo DRC, Libya, Misri na Afrika ya Kati.

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi wa Marekani kwa mwaka 2013 umefikia wastani wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2012. Hii imechangiwa na upungufu wa ajira na kushuka kwa soko la nyumba. Ukuaji wa uchumi wa Japan ulifikia asilimia 1.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2012. Hali hii imetokana na mafanikio ya jitihada za mabadiliko kwa kuongezeka usafirishaji wa bidhaa. Uchumi wa nchi za Ulaya umepanda kufikia *negative* 0.5 mwaka 2013 kutoka asilimia *negative* 0.7 mwaka 2012, hali hii imechangiwa zaidi na udhibiti wa matumizi ya bajeti.

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi wa China kwa mwaka 2013 umeendelea kubakia kama ulivyokuwa mwaka 2012 kwenye kiwango cha wastani wa asilimia 7.7. Hali hii imetokana na kuendelea kwa uwekezaji kulikochangiwa na ukuaji mdogo wa mikopo na kupanda kwa gharama za mitaji, uchumi wa nchi ya India umefikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2013, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2012, hii inatokana na kuongezeka kwa riba ambako kumeathiri sekta ya viwanda.

Ukuaji wa uchumi wa Afrika ya Kusini umefikia wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2013 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2012. hali hii imesababishwa na migogoro katika Sekta ya Madini na matatizo ya umeme.

Mwenendo wa Mfumko wa Bei Duniani

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei duniani imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2012. Kwa nchi zilizoendelea mfumo wa bei umeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 1.4 ikilinganishwa na asilimia 2 mwaka 2012. Nchi zinazoibuka kiuchumi na zinazoendelea umeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2013, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6 mwaka 2012. Hali hii inatokana na kupungua kwa shughuli za kiuchumi duniani, kushuka kwa bei za vyakula, kuendelea kwa utulivu wa bei za mafuta duniani na uwepo wa sera madhubuti za kifedha.

MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR

Ukuaji wa Pato la Taifa

Mhe. Spika, Pato la Taifa kwa Zanzibar lilifikia thamani ya shilingi 1,442.8 bilioni mwaka 2013 kwa bei za mwaka husika ikilinganishwa na thamani ya Shilingi 1,342.6 bilioni mwaka 2012. Ongezeko hili la Pato la Taifa limesababisha mafanikio ya ukuaji wa hali ya uchumi kwa wastani wa asilimia 7.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2012. Ukuaji huu mkubwa wa uchumi ambao haujawahi kutokea kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni, umetokana na sababu zifuatazo:-

1. Kuimarika kwa Sekta ya Kilimo, Misitu na Uvuvi ambayo imekua kutoka asilimia 2 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 3.6 mwaka 2013.
2. Kuimarika kwa baadhi ya sekta ya viwanda kulikochangiwa na ongezeko la ukuaji wa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia 0.1 mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2013.
3. Kuimarika kwa Sekta ya Huduma kulikochangiwa na ongezeko la ukuaji wa sekta ndogo za hoteli na mikahawa kutoka asilimia 0.2 mwaka 2012 hadi asilimia 6.5 mwaka 2013. Sekta ya Utawala wa Umma

kutoka asilimia 0.3 mwaka 2012 hadi asilimia 3.4 mwaka 2013. Na Sekta ya Elimu kutoka asilimia 1.2 mwaka 2012 hadi asilimia 3.5 mwaka 2013.

4. Kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 169,223 mwaka 2012 hadi kufikia watalii 181,301 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 7.1.
5. Kuendelea kwa hali ya amani na utulivu nchini.

Pato la Mwananchi

Mhe. Spika, Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 imeonesha kwamba, idadi ya wananchi wa Zanzibar imefikia watu 1,303,569 ambao wanakua kwa wastani wa asilimia 2.8. Kuongezeka kwa pato la taifa kwa zaidi ya ongezeko la watu kumepelekea kupanda kwa kiwango cha wastani wa pato la kila mtu, wastani wa pato la kila mtu limekua kwa asilimia 4.6 kutoka shilingi 1.03 milioni sawa na Dola za Kimarekani 656 mwaka 2012 kufikia shilingi 1.37 milioni au sawa na Dola za Kimarekani 667 mwaka 2013.

Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013 kasi ya ukuaji wa Sekta ya Kilimo imepanda kufikia wastani wa asilimia 3.6 kutoka wastani wa asilimia 2 mwaka 2012. Ongezeko hili limetokana na ukuaji wa Sekta ndogo ya Uvuvi iliyofikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2013, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2012 na Sekta ya Mazao iliyofikia ukuaji wa asilimia 3.6 mwaka 2013, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.7 mwaka 2012.

Mhe. Spika, ukuaji wa Sekta ya Huduma kwa mwaka 2013 umefikia asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2012. Ukuaji huo mdogo umesababishwa na kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ndogo ya usafiri na mawasiliano uliofikia asilimia 14.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 19.2 mwaka 2012. Sekta ya Biashara na Ukarabati ilifikia asilimia 7.7 mwaka 2013, ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2012. Sekta ya Afya imefikia asilimia 3.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2012.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Viwanda ukuaji wake umefikia asilimia 8.2 mwaka 2013, ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2012. Ukuaji huu mdogo ni kutokana na kupungua kwa ujenzi na uchimbaji mawe ambapo ujenzi ulifikia asilimia 10.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 14.2 mwaka 2012. Uchimbaji mawe umefikia asilimia 15.7 mwaka 2013, ikilinganishwa na asilimia 16.5 mwaka 2012. Aidha, sekta ndogo ya umeme, gesi na maji, ukuaji umefikia asilimia 3.7 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2012. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani imeongezeka kufikia asilimia 3.2 mwaka 2013 kutoka asilimia 0.1 mwaka 2012.

Mchango wa sekta katika Pato la Taifa

Mhe. Spika, Sekta ya Huduma ndio yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 44.1 mwaka 2013, kiwango hiki kimepungua kwa asilimia 2 ikilinganishwa na mchango wa wastani wa asilimia 45 mwaka 2012. Kupungua huko kumetokana na kupungua kwa sekta ndogo za biashara na ukarabati kutoka asilimia 9.5 mwaka 2012 hadi asilimia 9.3 mwaka 2013, Hoteli na Mikahawa kutoka asilimia 6.5. mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 6.3 mwaka 2013 na Taasisi za kifedha kutoka asilimia 2 mwaka 2012 hadi asilimia 1.9 mwaka 2013.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya kilimo mchango wake katika pato la taifa umefikia wastani wa asilimia 31 mwaka 2013; kiwango kimeongozeka kwa asilimia 0. 97 ikilinganishwa na mchango wa wastani wa asilimia 30.7 mwaka 2012. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya mazao kutoka asilimia 19.4 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 19.7 mwaka 2013.

Mhe. Spika, mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la taifa umefikia wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2013 kiwango hiki kimepungua kwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 11.3 mwaka 2012. Upungufu huu umetokana na kupungua kwa mchango wa sekta ndogo za uzalishaji viwandani kutoka asilimia 3.5 mwaka 2012 hadi asilimia 3.3 mwaka 2013 na sekta ndogo ya ujenzi kutoka asilimia 5.4 mwaka 2012 hadi asilimia 5.3 mwaka 2013.

Mfumko wa bei

Mhe. Spika, kasi ya Mfumko wa bei ilipungua kutoka asilimia 9.4 mwaka 2012 hadi asilimia 5 mwaka 2013. Kasi hii ya kushuka kwa mfumko wa bei nchini ilichangiwa na kushuka kwa mfumko wa bei za chakula hasa mchele na unga wa ngano kutoka asilimia 6.7 mwaka 2012 hadi asilimia 1.8 mwaka 2013 na mfumo wa bidhaa zisizo za chakula yaani Saruji, mafuta ya Petroli na dizeli kutoka asilimia 13. 2 mwaka 2012 hadi asilimia 8.5 mwaka 2013.

Kushuka huko kwa kasi ya mfumko wa bei nchini kulichangiwa sana na kushuka kwa bei za bidhaa muhimu za chakula na mafuta katika Soko la Dunia. Mafanikio haya ya kuendelea na tarakimu moja ni hatua nzuri kuelekea dhamira kuu ya serikali ya kuimarisha uchumi na kuinua kipato cha mwananchi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine serikali imeendelea na juhudi za kudhibiti mfumko wa bei kama ifuatavyo:-

(1) Kuendelea kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia pembejeo nafuu kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji nchini.
(2) Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kutoa elimu bora juu ya uzalishaji wenye tija.
(3) Kuendelea kupunguza ushuru katika bidhaa za chakula kama vile mchele, sukari na unga wa ngano kwa lengo la kusaidia wananchi kujikimu kimaisha.
(4) Kuendelea na jitihada za kuimairisha sekta ndogo ya nishati kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika.
(5) Kudhibiti upandaji wa bei usiokuwa wa lazima hasa kwa bidhaa za chakula ili kumuwezesha mwananchi kuimudu bei ya chakula.
(6) Kuendelea na mikakati ya kudhibiti bei ya mafuta nchini
(7) Kuendelea kuongezeka kwa waagizaji wa bidhaa nchini kutokana na kuondoa vikwazo vya biashara.

Biashara na Nchi za nje

Mhe. Spika, katika mwaka 2013 mwenendo wa biashara na nchi za nje umeimarika kutokana na kuongezeka wa thamani wa usafirishaji wa bidhaa. Hali hii imepelekea kushuka kwa nakisi ya biashara kwa asilimia 41kutoka nakisi ya shilingi 203,882.5 milioni mwaka 2012 hadi nakisi ya shilingi 120,252.3 milioni kwa mwaka 2013.

Mhe. Spika, thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 30 kutoka shilingi 67,390.5 milioni mwaka 2012 hadi kufikia thamani ya shilingi 87,799.6 milioni mwaka 2013. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la usafishaji wa mazao ya biashara kutoka thamani ya shilingi 63,160 milioni mwaka 2012 hadi shilingi 75,392.6 milioni mwaka 2013.

Aidha thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 23 kutoka thamani ya shilingi 271,273.1 milioni mwaka 2012 kufikia thamani ya shilingi 208,051.9 milioni kwa mwaka 2013. Kwa mwaka 2013 uagiziaji mkubwa ulikuwa katika vyombo vya usafiri na mashine.

Mhe. Spika, hata hivyo, uwiano wa pato la taifa na biashara za kimataifa umefikia wastani wa asilimia 21 mwaka 2013 kutoka wastani wa asilimia 25 mwaka 2012. Wakati uwiano wa pato la taifa na biashara za kimataifa kwa bidhaa na huduma umefikia wastani wa asilimia 43.2 wa mwaka 2013 kutoka wastani wa asilimia 55.3 kwa mwaka 2012.

Mhe. Spika, mwenendo huu wa uwiano wa pato la taifa na biashara za kimataifa bado hauridhishi kulingana na thamani ya pato la taifa na idadi ya watu nchini. Juhudi zaidi zinahitajika kuchukuliwa katika kuimarisha maingiliano ya kibiashara za kimataifa zikiwemo kuendelea kutekeleza mikakati ya usafirishaji, kuendelea kutoa nafuu maalum ya kodi ya forodha kwa mashine, vipuri na zana zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kutumika katika miradi mbali mbali ya maendeleo, kuitangaza Zanzibar zaidi kiutalii na uwekezaji kwa kushirikiana na Ofisi za balozi zilioko nje ya nchi na kushiriki maonesho mbali mbali ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvitangaza vivutio vya utalii na maeneo ya uwekezaji.

Mwenendo wa uingiaji wa Watalii

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013 mwenendo wa uingiaji wa watalii umeongezeka kwa asilimia 7.1 kufikia jumla ya watalii 181,301 mwaka 2013 kutoka watalii 169,223 mwaka 2012. Mwenendo huu mzuri wa watalii umetokana na idadi kubwa ya watalii walioingia kutoka Bara la Ulaya ambapo Italy walifikia idadi wa watalii 50,966 sawa na asilimia 28.1. Ujerumani walifikia watalii 14,891 sawa na asilimia 8.2. Uingereza walifikia watalii 13,763 sawa na asilimia 7.6 na Ufaransa walifikia watalii 12,542 sawa na asilimia 6.9.

Mwenendo mzuri wa uingiaji wa watalii umetokana na ongezeko la vivutio vya utalii nchini na kukamilika kwa miradi mikubwa ya hoteli kama Plan Hotel, Hide Away hotel, Larosa Hotel na White sands Hotel. Aidha kuongezeka kwa mtandao wa usafiri wa ndege yaani *(Network of Schedule flight)* kama vile First Jet, Shine Aviation na Zantaf Air wamefanya Zanzibar rahisi kufikika. Sababu nyengine ni hali ya amani na utulivu inayoendelea kuwepo nchini mwetu.

Mhe. Spika, uchambuzi wa mwenendo wa watalii wanaoingia nchini hauwiani na mwenendo wa matumizi wa fedha za kigeni yanayotokana na uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na mapato ya fedha za kigeni yanayotokana na utalii. Hali hii inatokana na upokeaji mdogo wa wageni kutoka Bara la Asia wakati matumizi makubwa ya bidhaa zinazotumika nchini hufanyika katika Bara hilo.

Hivyo, kuna haja ya kuitangaza zaidi Zanzibar katika nchi zenye idadi ndogo ya uingiaji wageni ili kuepukana na kutegemea watalii kutoka sehemu moja ambao inaweza kuleta athari za uchumi endapo nchi hizo zitakapopata matatizo, Mwenyezi Mungu aepushe mbali.

Ukuzaji wa rasilimali

Mhe. Spika, kwa ujumla thamani ya ukuzaji wa rasilimali imepungua kwa asilimia 10 kufikia shilingi laki mbili thalathini na tatu elfu mia nane tisini na moja milioni mwaka 2013 kutoka shilingi laki mbili hamsini na nane elfu mia tano tisini na tano milioni mwaka 2012. Hali hii imetokana na kupungua kwa uwekezaji katika eneo la vifaa vya usafiri na vifaa vyengine kutoka thamani ya shilingi laki moja ishirini na nane mia nane tisini na tisa ishirini na mbili milioni mwaka 2012 hadi kufikia shilingi 87,914 mwaka 2013.

Hata hivyo, thamani ya uwekezaji wa majengo umeongezeka kutoka shilingi 62,553 milioni mwaka 2012 hadi kufikia shilingi 64,883 milioni mwaka 2013. Uendelezaji wa ardhi na ujenzi wa barabara na madaraja umeongezeka kutoka shilingi 70,043 milioni mwaka 2012 hadi shilingi 72,408 milioni mwaka 2013.

Uwekezaji binafsi

Mhe. Spika, idadi ya miradi iliyoidhinishwa na mamlaka ya uwekezaji vitega uchumi Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 40 kutoka miradi 25 yenye thamani ya dola za kimarekani 50.09 milioni na kuzalisha ajira ya watu 1,123 mwaka 2012 hadi miradi 35 yenye thamani ya dola za kimarekani elfu moja na sitini na tisa nukta tisa milioni na kuzalisha ajira ya watu 1,165 mwaka 2013.

Maendeleo ya Kiuchumi

Mhe. Spika, matokeo mazuri ya ukuaji wa uchumi Zanzibar yameleta maendeleo ya kiuchumi na kuimarika kwa huduma za kijamii. Juhudi mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini zimesaidia sana katika kuimarika kwa hali ya ustawi wa kimaisha kwa wananchi wa Zanzibar. Miongoni mwa mafanikio ni haya yafuatayo:-

Kuongezeka kwa idadi ya wananchi waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa kutoka watu 8,721 mwaka 2012 hadi kufikia watu 10,684 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 22.5. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za msingi darasa la kwanza mpaka la saba za serikali na binafsi kutoka 240,122 mwaka 2012 kufikia 247,352 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 3.

Kuongezeka kwa uchapishaji wa vitabu vya wanafunzi ambapo jumla ya nakala 142,210 ya vitabu vilichapishwa. Aidha jumla ya nakala 3,820 ya vitabu vya viongozi vya walimu vimenunuliwa kwa masomo ya Sayansi, masomo

ya Sayansi jamii, Kiswahili na Kiingereza kuanzia darasa la kwanza hadi la nne. Pia vifaa vya maabara vilinunuliwa kwa ajili ya Skuli 113 za Sekondari.

Wastani wa uwiano wa walimu kwa wanafunzi kwa darasa la kwanza mpaka kidato cha nne kwa Skuli za Serikali na binafsi umefikia 1/26 kwa mwaka 2013 ikilinganishwa na wastani wa moja au ya mwalimu mmoja kwa wanafunzi 28 mwaka 2012.

Kuongezeka kwa asilimia 38 kwa wanafunzi waliopatiwa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 882 mwaka 2012/13 hadi wanafunzi 1,410 mwaka 2013/14.

Kuongezeka kwa ukuzaji rasilimali hasa katika shughuli za usafiri na mawasiliano, hoteli na mikahawa, uzalishaji viwandani, kilimo, uwindaji na misitu kutoka dola za kimarekani 59.1 milioni mwaka 2012 hadi kufikia dola za kimarekani bilioni 1.1.

Kuongezeka kwa watoa huduma katika sekta ya afya kama madaktari watoa huduma na wauguzi kutoka 1,880 mwaka 2012 hadi 2,375 mwaka 2013. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa madaktari kutoka 26 mwaka 2012 hadi 40 mwaka 2013. Watabibu kutoka 130 mwaka 2012 hadi 185 mwaka 2013.

Madaktari bingwa wa watoto kutoka 3 mwaka 2012 hadi 9 mwaka 2013. Wataalamu wa maabara kutoka 193 mwaka 2012 hadi 212 mwaka 2013. Wakunga wauguzi kutoka 472 mwaka 2012 hadi 526 mwaka 2013 na kadhalika.

Sekta ya fedha na huduma za benki

Mhe. Spika, sekta ya fedha imekuwa ni mojawapo ya sekta za kiuchumi ambazo zimekuwa zikipata mafanikio makubwa katika kipindi cha karibuni. Amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 18.4 kutoka shilingi mia nne na tatu nukta nne bilioni mwishoni mwa mwezi Machi mwaka 2013 ikilinganishwa na shilingi mia nne sabini na saba nukta saba bilioni kipindi kama hicho mwaka 2014. Hali hii inaashiria kuwa watumiaji wa huduma za kibenki wanaongezeka kutokana na uhamasishwaji unaoendelea unaotokana na ushindani wa benki.

Mhe. Spika, uchambuzi wa mikopo kwa walionufaika na mikopo hiyo inaonesha kuwa hadi mwezi Machi mwaka huu mikopo iliyotolewa ilifikia shilingi mia mbili na tatu nukta nane bilioni ambapo mikopo binafsi ilifikia asilimia 35.5. Biashara asilimia 20.5, Utalii asilimia 14.8, Mawasiliano na usafirishaji asilimia 4.9 na sekta zilizobakia zilikuwa chini ya asilimia 3.7 kila mmoja zikiwemo sekta za Kilimo na Viwanda ambazo hutoa mchango mkubwa katika uchumi.

Masuala ya Mtambuka Idadi ya Watu na Mgawanyo wake Kimikoa na kiumri Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sensa ya watu na Makaazi ya mwaka 2012 idadi ya watu wa Zanzibar imefikia 1,303,569 sawa na ongezeko la asilimia 2.8 kwa mwaka ambapo asilimia 46.3 ya watu hao wanaishi mijini na asilimia 53.7 wanaishi vijijini.

Kisiwa cha Unguja ndio chenye watu wengi zaidi waliofikia watu 896,721 sawa na asilimia 68.8 ikilinganishwa na Kisiwa cha Pemba chenye watu 406,848 sawa na asilimia 31.2.

Mhe. Spika, mgawanyo wa watu Kimikoa unaonesha kwamba idadi kubwa inapatikana katika Mkoa wa Mjini Magharibi wenye jumla ya watu 593,678 sawa na asilimia 45.5 ya Wazanzibari wote, ukifuatiwa na Mkoa wa Kaskazini Pemba wenye watu 2,011,732 sawa na asilimia 16 ya Wazanzibari wote. Mkoa wenye watu kidogo zaidi ni Mkoa wa Kusini Unguja wenye watu 115,588 sawa na asilimia 8.9 ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa hizo za Sensa ya mwaka 2012 karibu nusu ya Wazanzibari au asilimia 46 wapo katika Mkoa wa Mjini Magharibi hali iliyopelekea Mkoa wa Mjini Magharibi kuwa na msongamano mkubwa wa watu kiasi cha kufikia watu 2581 kwa kila mita moja ya mraba. Hali hii ina athari kubwa katika mipango bora ya miji na matumizi endelevu ya rasilimali hususan rasilimali ardhi.

Katika hili serikali inaendelea kuchukua juhudi maalum kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na uandaaji mpango mpya wa mji, kuangalia uwezekano wa kufanya tafiti zitakazotathmini athari za kuongezeka kwa watu na kuibua mikakati endelevu ya kupunguza ukubwa wa tatizo.

Mhe. Spika, kwa upande wa mgawanyo wa idadi ya watu kiumri; taarifa zinaonesha kwamba idadi kubwa ni ya watoto chini ya miaka 15 waliofikia 554,349 sawa na asilimia 42.5 ikifuatiwa na vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 waliofikia 265,103 sawa na asilimia 20.3 ya Wazanzibari wote. Mgawanyo huu unaonesha kwamba Zanzibar ina jumla ya watu laki nane kumi na tisa elfu mia nne hamsini na mbili sawa na asilimia 62.8 ambao ama ni watoto au vijana ambao wengi wao ni wategemezi katika familia zao.

Aidha jumla ya watu 36,726 sawa na asimilia 2.8 ya idadi ya watu wa Zanzibar ni wazee wenye umri wa miaka 65 na zaidi. Hali hii inamaanisha kwamba Zanzibar ina idadi kubwa ya utegemezi hususan ikizingatiwa kwamba vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 24 ingawa ni sehemu ya nguvu kazi wengi wao bado ni wanafunzi na maisha yao yanategemea nguvu ya familia zao.

Mhe. Spika, tafsiri halisi ya vijana kwa mujibu wa sera ya vijana ya Zanzibar inatambua kwamba vijana kuwa ni watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Kutokana na tafsiri hii, vijana wa Zanzibar wamefikia watu 446,927 sawa na asilimia 34.3 au theluthi moja ya Wazanzibari wote. Kundi hili la vijana endapo halijawekezwa vizuri linaweza kuzaa athari kubwa kijamii na kiuchumi nchini. Kwa hali hii kuna haja kubwa kwa Serikali kuwekeza katika kuwajengea uwezo vijana kielimu na kiuchumi ili wawe rasilimali yenye tija kwa taifa kuliko kuwa athari au kikwazo kiuchumi na kijamii kama inavyojitokeza katika nchi nyingi duniani.

Mhe. Spika, uwekezaji wa vijana kwa Zanzibar ni pamoja na kuimarisha mafunzo ya Amali, kuimarisha wigo wa mikopo ya Elimu ya Juu, kuongeza upatikanaji mitaji kwa njia ya mikopo ya masharti nafuu, kukuza uwekezaji wenye kuzaa ajira nyingi zaidi, uvuvi wa bahari kuu n.k. Ili kulifanikisha hili, vijana hawana budi kuelimishwa zaidi ili waende sambamba na dhamira ya Serikali yao.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 35 na miradi 75 ya maendeleo kupitia Klasta tatu zinazounda MKUZA II ambapo programu moja na miradi tisa ni mipya. Jumla ya TZS 305.4 bilioni zilitengwa kwa madhumuni hayo. Kati ya fedha hizo TZS 70.0 bilioni sawa na asilimia 23 ni kutoka Serikalini na TZS 235.4 bilioni sawa na asilimia 77 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ruzuku ni TZS 86.8 bilioni na mkopo ni TZS 148.6 bilioni.

UTEKELEZAJI WA MAENEO YALIYOPEWA KIPAUMBELE

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014, maeneo yaliyopewa kipaumbele yalikusudia kuleta mageuzi ya Serikali na kiuchumi, kujenga uwezo wa rasilimali watu pamoja na kuzingatia masuala mtambuka kwa lengo la kukuza uchumi. Utekelezaji wa maeneo yaliyopewa kipaumbele kisekta ni kama ifuatavyo:

Kuimarisha Sekta ya Utalii

Mhe. Spika, kamati za utalii katika kila wilaya zimeanzishwa na zimejengewa uwezo ili ziweze kusimamia masuala ya utalii kwa wote. Mkutano wa wananchi na viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ulifanyika kujadili namna ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu vinavyofanyika katika maeneo ya utalii. Aidha, hatua za ujenzi wa vituo vya kutoa taarifa za utalii za usalama zimeanza ambapo michoro ya ramani ya vituo imeandaliwa. Matengenezo ya Kasri la Forodhani yamefanyika pamoja na uungaji wa umeme na ujenzi wa kisima na choo katika maeneo ya Mangapwani na Chemba ya Watumwa ili kuimarisha vivutio vya utalii. Aidha, Serikali katika kuipeleka hatua nyengine sekta hii imetayarisha Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii kwenye maabara ambayo wadau wa Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na wasomi walishiriki.

Kuimarisha Sekta ya Biashara

Mhe. Spika, katika kuimarisha usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, Utafiti wa *Brand blueprint* na *brand expression* umekamilika kwa hatua ya awali kwa kuanzia na aina nne za bidhaa za viungo (Karafuu, Mdalasini, Pilipili manga na Pilipili hoho) ambapo matayarisho ya uzinduzi wa awamu ya majaribio kwa *branding* ya bidhaa za viungo yanaendelea. Vile vile, hatua za utambulisho kwa zao la karafuu zinaendelea na tayari jina na alama husika zimeainishwa. Aidha, Serikali katika kuweka mazingira bora ya sekta hii imetayarisha Programu ya Kuimarisha Mazingira Bora ya Biashara kwenye maabara ambayo wadau wa Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na wasomi walishiriki.

Kuimarisha Sekta ya Viwanda

Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za kuwavutia wawekezaji wa viwanda nchini pamoja na kutoa vivutio maalum kwa wawekezaji wa sekta hiyo vikiwemo kuweka miundombinu ya barabara, umeme na maji katika maeneo ya uwekezaji, kutoa msamaha wa kodi kwa mitambo na mashine pamoja na kurahisisha upatikanaji wa ardhi.

Hatua nyengine ni maandalizi ya Sera ya Viwanda ambapo Serikali imeandaa taarifa maalum ya ushindani kiviwanda *(Tanzania Industrial Competitivement Report TICR 2012)* ambayo inalinganisha ushindani kiviwanda kwa upande wa Zanzibar na nchi za visiwa kama Mauritius, Sychelles na nchi nyenginezo. Hatua hii ni ya awali na imeibua maeneo muhimu katika maandalizi ya Sera ya Viwanda na Mkakati wa Maendeleo wa Viwanda *(Industrial Development Strategy)*.

Aidha, katika kuendeleza ujasiriamali *(SME/entrepreneurship development)*, Serikali imeandaa vigezo maalum vya kutoa usaidizi kwa wajasiriamali vikiwemo; kuwa na usajili rasmi, akaunti ya benki na kuwa katika sekta ya uzalishaji na usarifu wa bidhaa.

Kuimarisha Sekta ya Kilimo

Mhe. Spika, kilimo cha umwagiliaji maji kiliimarishwa kwa kuongezwa miundombinu ya umwagiliaji kutoka mita 500 kufikia mita 800. Ununuzi wa mbolea zisizo na kemikali umefanyika. Elimu kwa wakulima kupitia skuli za wakulima inaendelea kutolewa. Jumla ya tani 900 za mbolea aina ya UREA na tani 150 za TSP zilisambazwa kwa wakulima wa mpunga Unguja na Pemba. Kiwango cha mpunga uliozalishwa kimeongezeka kufikia tani 33,655 mwaka 2013 ikilinganishwa na tani 6,372 mwaka 2012 sawa na asilimia 428.

Aidha, uzalishaji wa mazao ya mahindi umeongezeka kutoka tani 857 mwaka 2012 hadi kufikia tani 1,419 mwaka 2013 sawa na asilimia 65.5 na viazi vitamu kutoka tani 31,768 mwaka 2012 hadi kufikia tani 53,657 mwaka 2013 sawa na asilimia 68.9. Ongezeko hili limetokana na hali nzuri ya hewa, ongezeko la eneo la uzalishaji na matumizi mazuri ya pembejeo. Utayarishaji miongozo ya uendeshaji wa uhifadhi wa chakula umekamilika kwa hatua ya mwanzo na mafunzo kwa wajasiriamali juu ya upotevu wa mazao yamefanyika ili kusaidia juhudi za kuimarisha usarifu wa mazao.

Kuimarisha Utawala Bora

Mhe. Spika, hatua za kuandaa Sera na Mpango Mkakati wa Kupambana na Rushwa na Kuhujumu Uchumi zimeanza. Warsha za uhamasishaji wa kupambana na rushwa zimefanyika kwa viongozi waandamizi wa Serikali na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Aidha, mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu masuala ya fedha haramu yamefanyika ili kufanikisha juhudi za kuzuia rushwa na kuhujumu uchumi.

Kuimarisha Huduma za Afya

Mhe. Spika, katika kuendeleza kupandisha hadhi vituo vya afya, matengenezo ya chumba cha upasuaji Hospitali ya Kivunge yamekamilika sambamba na upatikanaji wa vifaa vyake. Aidha, matengenezo ya wodi ya wanawake katika Hospitali ya Micheweni yanaendelea na ujenzi wa wodi mbili kwa jengo jipya la hospitali hiyo yameanza. Ununuzi wa dawa muhimu kwa wananchi umefanyika pamoja na upatikanaji wa vifaa tiba.

Katika kupunguza vifo vya mama na watoto, ujenzi wa wodi ya wazazi na watoto kwa Hospitali ya Wete umekamilika na ujenzi wa Kituo cha Afya Mwera umefikia hatua za mwisho kukamilika. Kazi ya upigaji wa dawa na kuua viluilui vya malaria imefanyika katika Wilaya za Mjini na Magharibi sambamba na ukusanyaji wa mbu katika maeneo maalum 22 yaliyochaguliwa Unguja na Pemba. Kazi za uhamasishaji wa utoaji ushauri nasaha na upimaji wa hiari imefanyika katika Wilaya za Kati Unguja na Micheweni Pemba kwa ajili ya kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI.

Kuimarisha Ubora wa Elimu

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira mazuri ya ufundishaji, ujenzi wa madarasa 118 ya skuli za msingi umekamilika ambapo Unguja 66 na Pemba 52. Ujenzi wa skuli za maandalizi za Jongowe na Konde umekamilika. Ukamilishaji wa madarasa ya msingi na maandalizi umekwenda sambamba na uchongaji wa madawati 1,800 na seti za meza na viti 144. Ujenzi wa vyoo, sehemu za kunawia mikono, minara na matangi ya kuhifadhia maji katika skuli tano za msingi umekamilika kwa Unguja na nane kwa Pemba.

Vile vile, ujenzi wa skuli za Sekondari za Tunguu umekamilika, Kibuteni umefikia asilimia 45 na Mkanyageni asilimia 75. Aidha, maabara za skuli za Sekondari Unguja na Pemba zimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa mbali mbali. Taratibu za zabuni kwa ajili ya uchapishaji vitabu vya kiada na miongozo ya walimu kwa masomo ya Kiingereza, Hisabati, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Jiografia na Sayansi zinaendelea. Uandishi wa moduli ya nane ya kutolea mafunzo kwa wakufunzi wa walimu wa maandalizi kwa njia ya redio umeendelezwa. Mafunzo mbali mbali ya walimu kazini yamefanyika yakiwemo ya kufundisha kwa njia ya mjumuisho, taaluma ya takwimu na mafunzo kazini kwa walimu wa Sayansi.

Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na uhifadhi wa mazingira

Mhe. Spika, uandaaji wa kitini kwa ajili ya kufundishia mabadiliko ya tabia nchi umeendelea. Mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi umekamilika na kupitishwa. Kazi ya uhifadhi wa mazingira imeendelea kwa kuweka usimamizi endelevu wa maliasili ambapo jumla ya doria 47 zimefanyika ili kukabiliana na waharibifu wa mazingira. Vile vile, doria 70 zimefanyika katika kukabiliana na utumiaji wa mifuko ya plastiki na watu 31 wamefikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Kuendelea kushirikisha makundi yote katika kuleta maendeleo

Mhe. Spika, ili kushirikisha kikamilifu makundi yote katika kuleta maendeleo, Sera ya Jinsia inatayarishwa na ipo katika hatua za mwisho kukamilika na jumla ya kamati 114 za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia zimeundwa katika shehia mbali mbali Unguja na Pemba. Miongozo miwili ya dini imeandaliwa yenye lengo la kushajihisha jamii juu ya kupinga na kuachana na vitendo vya udhalilishaji. Aidha, Sera ya Hifadhi ya Jamii imepitishwa Serikalini na mchakato wa mapitio ya Sera ya Vijana, Sera ya Uwezeshaji na Sera ya Ushirika pamoja na uandaaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unaendelea. Jumla ya mikopo 212 yenye thamani ya TZS 144.87 milioni ilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wadogo 317 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kutekeleza vipaumbele vilivyotangulia, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa haraka na ufanisi zaidi, Serikali ilitekeleza visaidizi mbali mbali vikiwemo kuimarisha mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma na miundombinu.

Kuimarisha Mahusiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Mhe. Spika, katika kushirikisha sekta binafsi katika maendeleo ya kiuchumi, maandalizi ya Sera, Sheria na Miongozo ya Mashirikiano ya Sekta za Umma na Binafsi yameanza kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa ukusanyaji wa maoni ya wadau wa sekta mbali mbali. Ziara ya mafunzo kwa maafisa wanne imefanyika kwa ajili ya kupata uzoefu wa kuimarisha mahusiano ya sekta ya umma na sekta binafsi nchini.

Kuimarisha Miundombinu

Mhe. Spika, katika kuimarisha miundombinu muhimu ya usafiri, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zinazoingia mjini za Fuoni na Bububu umekamilika na mapitio ya Upembuzi Yakinifu kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri yanaendelea.

Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na wawekezaji wa Uturuki kwa ajili ya kufanya matengenezo ya uwanja wa ndege wa Pemba. Kwa upande wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kazi zinazoendelea kwa mradi wa ujenzi wa njia ya kupitia ndege ni kukamilisha njia za kupitia ndege na maegesho ya ndege ambazo zinatarajiwa kukabidhiwa Serikalini katika mwezi wa Oktoba 2014. Aidha, kuhusu ujenzi wa jengo jipya la abiria ujenzi huu sasa unaendelea na unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa Septemba 2015.

Uwezekano wa kuwa na Nishati Mbadala na Endelevu

Mhe. Spika, mchakato wa kufanya upembuzi yakinifu katika masuala ya nishati mbadala unaendelea kwa mashirikiano na Umoja wa Ulaya ambapo utambuzi wa maeneo matano (matatu Unguja na mawili Pemba) umefanyika kwa kuwekewa vifaa vya ukusanyaji wa takwimu muhimu za upepo ili kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme wa upepo na jua.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 6 Mei, 2014 imetiliana saini na Umoja wa Ulaya Mkataba wa Fedha wa kusaidia utafutaji nishati mbadala. Vile vile, maeneo ya huduma za kijamii zikiwemo skuli, hospitali, misikiti na madrasa katika vijiji mbali mbali Unguja na Pemba yamefungiwa vifaa vya umeme wa jua kwa majaribio na mafunzo juu ya matumizi ya nishati mbadala kwa vijiji hivyo yanaandaliwa. Aidha, taratibu za kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti Nishati na Maji zinaendelea.

Upatikanaji wa Maji Safi na Salama

Mhe. Spika, matengenezo ya miundombinu ya usambazaji wa maji kwa ajili ya kuzuia upotevu wa maji yamefanyika katika maeneo ya Magogoni, Kiembesamaki, Makadara na Mji Mkongwe kwa Unguja na Chake Chake Mjini kwa Pemba. Vile vile, utafiti wa mahitaji na usambazaji wa maji umekamilika kwa eneo la Tumbe na kwa upande wa Nungwi utafiti unaendelea.

Utekelezaji Kifedha

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Programu na Miradi ya Maendeleo ilipangiwa jumla ya TZS 305.4 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 70.0 bilioni zilitarajiwa kutolewa na Serikali na TZS 235.4 bilioni zilitarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi mwezi Machi 2014, jumla ya TZS 129.7 bilioni zilitolewa sawa na asilimia 43 ya bajeti, ambapo TZS 27.7 bilioni zilitolewa na Serikali sawa na asilimia 40 na TZS 101.9 bilioni sawa na asilimia 43 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, upatikanaji wa kiwango hiki cha fedha kwa miezi tisa kwa mwaka 2013/2014 ni pungufu ya TZS 72.0 bilioni sawa na asilimia 35.7 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2012/2013 katika kipindi kama hicho ambapo TZS 201.7 bilioni zilipatikana. Kwa upande mwengine, kiwango hiki cha fedha ni asilimia 42.5 ikilinganishwa na asilimia 59.1 kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, Klasta ya Ukuzaji Uchumi na Upunguzaji Umasikini wa Kipato ilitekeleza jumla ya programu 18 na miradi 25. Jumla ya TZS 120.4 bilioni ya bajeti zilitengwa. Serikali ilitenga TZS 38.3 bilioni na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia TZS 82.0 bilioni ya bajeti. Aidha, ruzuku ni TZS 23.0 bilioni na mkopo ni TZS 59.0 bilioni. Kufikia Machi 2014, jumla ya TZS 59.3 bilioni sawa na asilimia 49 zilipatikana kwa kutekeleza programu na miradi iliyo katika klasta hii. Kati ya fedha hizo, TZS 15.9 bilioni sawa na asilimia 42 kutoka Serikalini na TZS 43.3 bilioni sawa na asilimia 53 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii ina jumla ya programu 11 na miradi 29 ya maendeleo ya kutekelezwa kwa gharama ya TZS 161.4 bilioni. Serikali ilitenga TZS 18.0 bilioni na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia TZS 143.3 bilioni. Aidha, ruzuku ni TZS 54.8 bilioni na mkopo ni TZS 88.5 bilioni. Kufikia

Machi 2014, jumla ya TZS 62.4 bilioni sawa na asilimia 39 ya bajeti ya Klasta zilipatikana. Kati ya hizo, Serikali imetoa TZS 5.8 bilioni sawa na asilimia 32 ya fedha iliyojipangia na Washirika wa Maendeleo walichangia TZS 56.6 bilioni sawa na asilimia 39 ya fedha zilizopangwa.

Mhe. Spika, Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa ilitekeleza jumla ya programu sita na miradi 21 yenye jumla ya TZS 23.6 bilioni sawa na asilimia 7.7 ya bajeti ya maendeleo katika mwaka 2013/14. Serikali ilitenga TZS 13.6 bilioni na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia TZS 10.0 bilioni. Fedha zilizotolewa kwa kipindi cha miezi tisa cha Julai-Machi ni TZS 8.0 bilioni sawa na asilimia 34 ya bajeti ya Klasta. Kati ya fedha hizo Serikali imechangia TZS 6.0 bilioni sawa na asilimia 44 ya fedha iliyojipangia na Washirika wa Maendeleo walichangia TZS 2.0 bilioni sawa na asilimia 20 ya fedha zilizopangwa.

Changamoto za Utekelezaji

Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka wa 2013/2014 umeonesha changamoto ambazo ni pamoja na mchango wa sekta za viwanda katika pato la taifa kuwa mdogo. Juhudi zaidi bado zinahitajika kuiendeleza sekta hii ili kuongeza ajira na kukuza pato la taifa. Aidha mapato ya ndani bado ni madogo na hutumika zaidi kwa kazi za kawaida. Hii inapelekea kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kwa wakati uliopangwa.
Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2014;

Uchumi wa Dunia na Mwelekeo wa Uchumi Duniani

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Benki ya Dunia kasi ya ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka kufikia asilimia 3.6 mwaka 2014. Uchumi wa nchi zilizoendelea nao unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.2 mwaka 2014. Hali hii inatokana na kumalizika kwa kipindi cha kuzorota kwa uchumi katika nchi za Ulaya, kukua kwa soko la ajira, kurejeshwa kwa mikopo ya nyumba na kuongezeka maradufu usafirishaji pamoja na utulivu wa bei za vyakula, mafuta pamoja na madini.

Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi zinatarajiwa kuwa katika hali ya mchanganyiko. Kushuka na kupanda kwa baadhi ya nchi kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nje kutoka nchi zilizoendelea baada ya kurejea kwa hali nzuri ya uchumi, sambamba na kuendeleza sera za kudhibiti hali ya fedha katika nchi hizo.

Mfumko wa Bei Duniani

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei duniani inatarajiwa kushuka hadi asilimia 3.5 mwaka 2014 ambapo nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi zinatarajiwa kushuka hadi asimia 5.5 mwaka 2014. Hii ni kutokana na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kupungua kwa mahitaji ya ndani katika nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi. Hata hivyo, kasi ya mfumko wa bei kwa nchi zilizoendelea unatarajiwa kupanda kufikia asilimia 1.5 mwaka 2014 kutokana na kupungua kwa tatizo la ajira.

Hali ya Uchumi wa Zanzibar - Matarajio ya Ukuaji kwa mwaka 2014

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2014 unatarajiwa kuimarika zaidi. Utekelezaji wa malengo ya uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa dira ya maendeleo ya 2020, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini awamu ya pili, malengo ya *millennium* ya mwaka 2015 pamoja na mageuzi ya msingi na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014 uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.8 kutoka ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2013.

Mambo Yatakayoleta Ukuaji Uchumi

Mhe. Spika, matarajio ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2014 yanatokana na mambo yafuatayo:-

1. Kuimarika kwa sekta ya utalii kutokana na kuanza kwa utekelezaji wa programu ya mjumuisho ya kuendeleza utalii kama ilivyotayarishwa kutoka maabara.

2. Kuimarisha mazingira ya biashara kutokana na uwekezaji wa programu mazingira ya biashara.
3. Kuimarika kwa vyanzo vya mapato kutokana na mkakati wa utafutaji wa raslimali fedha
4. Kuanza utekelezaji wa miradi ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi
5. Kuendelea kuimarisha amani na utulivu wa kisiasa pamoja na uwajibikaji.
6. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri, umeme, maji na mawasiliano.
7. Kuendelea kuimarisha hali ya raslimali watu.
8. Matokeo ya hali ya hewa nzuri ambayo itaongeza uzalishaji katika sekta za kilimo na uvuvi.
9. Kuimarika kwa miundo ya kilimo hasa cha umwagiliaji maji.

Mfumko wa Bei

Mhe. Spika, pamoja na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar, mfumko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika tarakimu moja. Matarajio haya ni kutokana na matarajio ya kushuka kwa mfumko wa bei duniani na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa mazao ya chakula na biashara. Kuimarika kwa sekta uvuvi na kuendelea kuimarika kwa thamani ya sarafu ya Tanzania.

Mwelekeo ya Mpango wa Maendeleo wa 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015 mwelekeo wa mpango wa maendeleo utaendelea kuzingatia utekelezaji wa dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2020, ikiwa malengo ya kujenga jamii iliyoelimika kwa elimu bora na inayotoa wataalamu wenye hadhi ya kimataifa yenye siha iliyoimarika kiuchumi na inayojali umoja wa kitaifa na kufuata misingi ya utawala bora. Vile vile utazingatia mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUZA 2), mpango wa utekelezaji wa miaka mitano wa MKUZA 2, malengo ya maendeleo ya *millennium* ya 2015 na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015.

Maeneo ya Kipaumbele 2014/2015

Mhe. Spika, serikali itaendelea na juhudi za kukuza uchumi kwa kasi zaidi na kuongeza ajira hususan kwa vijana. Katika kufikia azma hiyo, serikali imekusudia kuendelea na jitihada za kuleta mageuzi ya kiuchumi na serikali ili kufikia malengo ya MKUZA 2 na dira ya maendeleo ya Zanzibar 2020. Kwa mwaka 2014/2015 mkazo utawekwa katika maeneo yafuatayo:-

a) Kutekeleza programu ya kuimarisha utalii, programu ya kuimarisha mazingara ya biashara na mkakati wa utafutaji wa raslimali fedha na uimarishaji wa sekta ya umma na sekta binafsi iliyoibuliwa kwenye maabara. (*Results for Prosperity- R4P*);
b) Kufanya tafiti mbali mbali katika sekta zote zitakazosaidia utoaji sahihi wa maamuzi na upangaji wa mipango ya maendeleo;
c) Kuimarisha miundombinu hasa usafiri wa baharini kwa ununuzi wa meli, barabara na kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria la Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar;
d) Kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo kutoa elimu bora, huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama; na
e) Kuimarisha huduma kwa makundi maalum hususan kwa wazee wasiojiweza, watoto na wenye ulemavu.

Mwelekeo wa Programu na Miradi 2014/2015

Mhe. Spika, serikali itaendelea kutekeleza programu na miradi mbali mbali ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara, anga na majini. Kwa upande wa barabara, serikali itaendelea na ujenzi wa barabara za Ole/Kengeja, Wete/Gando na Wete/Konde kwa Pemba na barabara tatu za vijijini Unguja, Koani/Jumbi, Kizimbani/Kiboje na Jendele/Cheju Kaebona.

Kwa upande wa usafiri wa anga, serikali itaendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume. Eneo la maegesho ya ndege na kuweka vifaa na mitambo. Aidha itaendeleza ujenzi wa taa za kuongozea ndege na miundombinu ya maji.

Kwa upande wa usafiri wa majini, serikali itaendelea na azma ya kujenga bandari yenye kina kirefu kwa ajili ya kuhudumia meli za mizigo kufuatia upatikanaji wa fedha za mradi huu. Aidha, serikali itaendelea kulipa malipo ya utengenezaji wa meli ya serikali ili kurahisisha usafiri wa baharini kwa wananchi.

Mhe. Spika, kuhusu kilimo, serikali itaendelea kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, madawa ya magugu na huduma za matrekta. Aidha, serikali itaendeleza programu na miradi ya kuimarisha miundombinu na umwagiliaji, kutoa mafunzo ya uhifadhi na usarifu wa mazao kwa wakulima, kuendeleza tafiti za mazao ya chakula na biashara na matayarisho ya ujenzi wa dakhalia katika Chuo cha Kizimbani.

Vile vile serikali itaendelea na mradi wa kuimarisha zao la karafuu na kuzalisha miche milioni moja ya mikarafuu na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo.

Kwa upande wa uvuvi, serikali itaendeleza juhudi za kuongeza ajira kwa vijana kwa kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini na kujenga soko jipya la samaki na diko Malindi.

Kwa sekta ya mifugo, serikali itaendelea na programu ya miundombinu ya ufugaji kwa kumaliza ujenzi wa josho Mjimbini na kituo cha kutoa huduma za mifugo Unguja-Ukuu.

Mhe. Spika, kuhusu nishati, serikali itaendelea na juhudi za kufanya utafiti wa vyanzo mbadala vya umeme na kutayarisha programu ya nishati endelevu. Vile vile itaendelea na usambazaji wa umeme vijijini kwa upelekaji wa umeme katika visiwa vya Kisiwapanza na Makoongwe Pemba.

Aidha katika kuimarisha huduma za miji, serikali itaendelea na kujenga ukuta wa ukingo wa bahari Mizingani na kujenga michirizi ya maji ya mvua. Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa kuendelea na programu ya ujenzi wa ofisi za serikali na pia kuendelea na programu ya mageuzi katika usimamizi wa fedha na programu ya upatikanaji wa raslimali fedha.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya utalii, serikali itatekeleza programu mjumuisho ya utalii inayolenga kuongeza vivutio, huduma, masoko, utawala, miundombinu na mazingira ili sekta hii izidi kuongeza mapato na ustawi wa wananchi. Aidha sekta ya biashara itatekeleza programu ya mazingira bora ya biashara yenye lengo la kurahisisha ufanyaji wa biashara na kuimarisha taasisi ya viwango kwa kuanza na ujenzi wa ofisi, maabara na upatikanaji wa vifaa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za ustawi wa jamii, kwa upande wa elimu, serikali itaendeleza raslimali watu na ujuzi kwa kuajiri walimu waliohitimu shahada na stashahada katika masomo ya sayansi, hisabati, jiografia, historia na Kiingereza kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika elimu.

Aidha, itaendeleza uimarishaji wa elimu ya msingi kwa kuanza ujenzi wa skuli 10 za ghorofa na kuchapisha vitabu vya madarasa ya tano na sita vya masomo kumi na mbili.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya afya, serikali itaendelea kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa kwa kuimarisha miundombinu ya afya, kufanya matengenezo ya jengo la kiwanda cha madawa kwa ajili ya utoaji wa huduma za mama na watoto, kujenga wodi mpya ya watoto na kadhalika. Aidha serikali itaendelea na azma yake ya kuipandisha hadhi Hospitali ya Abdalla Mzee kuwa ya Mkoa kwa kuanza ujenzi wa hospitali hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuhusu sekta ya maji, serikali itaendeleza jitihada zake za kuimarisha maji mijini kwa kubadilisha mabomba machakavu na kuweka mabomba mapya ya maji katika eneo la Mji Mkongwe, uchimbaji wa visima na ufungaji wa mita. Aidha kwa upande wa maji vijijini Unguja na Pemba, serikali itaendelea na uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba na upelekaji wa umeme.

Mhe. Spika, katika kuendeleza utawala bora na umoja wa kitaifa, serikali itaendelea na kutekeleza programu ya TASAF katika mpango wa uhaulishaji wa fedha *(cash transfer)* kwa kaya maskini 2,256 za Zanzibar.

Aidha, katika kuimarisha sekta za sheria, serikali itaendelea na mageuzi ya sekta ya sheria, matengenezo ya majengo ya Mahakama ya Chake-Chake pamoja na uimarishaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Serikali itaendelea kuimarisha takwimu kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya na kuwajengea uwezo watakwimu. Aidha, serikali itaendelea na ujenzi wa kituo cha kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya Kidimni.

Rasilimali ya Utekelezaji wa Mpango kwa mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, mpango wa maendeleo 2014/2015 unalenga kutekeleza jumla ya programu 32 na miradi 57 ya maendeleo kupitia *clusters* tatu za MKUZA 2 ambapo programu tatu ni mpya zilizotokana na maabara ya utalii, mazingira bora ya biashara na utafutaji wa raslimali fedha. Na miradi sita ni mipya.

Mpango huu unatarajia kutumia jumla ya shilingi 331.3 bilioni kwa ajili ya kugharamia programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Serikali itatoa shilingi 65.9 bilioni, sawa na asilimia 20 ya bajeti yote ya maendeleo na shilingi 265.4 bilioni, sawa na asilimia 80 kutoka kwa washirika wa maendeleo ambapo ruzuku ni shilingi 66.3 bilioni na mikopo ni shilingi 199.1 bilioni.

Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji

Mhe. Spika, kazi za ufuatiliaji na tathmini kwa programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/2014 zilifanyika kupitia mpango mkuu wa ufuatiliaji wa MKUZA 2 kwa kuhakikisha wadau mbali mbali kupitia ngazi tofauti za utaratibu na utekelezaji.

Tume ya Mipango kwa kushirikiana na wizara, idara na taasisi zinazojitegemea zilifanya ziara za kutembelea utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa vipindi vya robo mwaka na taarifa za kina za ufuatiliaji zilitayarishwa na kusambazwa kwa wadau ikiwa ni miongozo ya utekelezaji kwa kipindi kijacho.

Mhe. Spika, kazi nyengine zilizofanyika ni pamoja na utayarishaji wa taarifa ya mwaka 2012/2013 ya utekelezaji wa MKUZA 2, utayarishaji wa mapitio ya sekta ya fedha, kusaidia mikutano na kamati za ufuatiliaji. Mafunzo mbali mbali kwa maafisa mipango juu ya ufuatiliaji na tathmini. Aidha maandalizi ya utayarishaji wa ripoti ya malengo ya maendeleo ya *millenium* ya mwaka 2013 na mapitio ya sekta ya kilimo yameanza.

Mhe. Spika, halikadhalika kwa ajili ya kuimarisha majukumu na kazi za ufuatiliaji na tathmini ya MKUZA, Tume ya Mipango inaendelea na uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya MKUZA 2 ambapo tathmini ya mahitaji ya ufuatiliaji yamefanyika katika wizara, idara na taasisi zinazojitegemea, tawala za mikoa na taasisi za kiraia pamoja na warsha na mijadala ya kitaifa imefanyika kote Unguja na Pemba.

Kukamilika kwa mfumo huu kutasaidia kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji kwa ajili ya utayarishaji wa mipango na bajeti zenye kuleta matokeo mazuri na haraka. Vile vile mfumo huu utasaidia kuandaa programu na miradi yenye mfumo wa matokeo ambapo Tume ya Mipango itaweza kupima viashiria vya programu na miradi ili kuweza kufuatilia utekelezaji wake kwa urahisi zaidi.

Hitimisho

Mhe. Spika, mwelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo ulioelezwa unahitaji umahiri wa sote kwa pamoja kuutekeleza. Hii ikiwa ni pamoja na kutekeleza programu zilizoibuliwa katika maabara ambazo ni programu mjumuisho; ya kuendeleza utalii Zanzibar, programu ya kuweka mazingira bora ya biashara na programu ya utafutaji wa raslimali fedha.

Utekelezaji mzuri wa programu hizi utazidisha kuitangaza Zanzibar ili kubaki katika ramani ya utalii na kituo cha biashara kwa kurahisisha ufanyaji wa biashara nchini, pamoja na kuvutia miradi ya ubia wa sekta ya umma na binafsi. Na hatimaye kuongeza mapato kwa kuendeleza nchi na wananchi wake.

Aidha, serikali itaendelea na nia ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini kwa kuendeleza kuwekeza katika maendeleo ya watu, kuimarisha miundombinu na utawala bora ili maendeleo endelevu yaweze kupatikana.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuzidi kusisitiza kwamba masuala yatakayopewa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha, serikali kwa upande wake itafanya jitihada ya kutafuta raslimali fedha ili maeneo hayo yaweze

kutekelezwa kwa ufanisi. Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi na wananchi katika utekelezaji wa sera na mipango ya nchi ikijumuisha utunzaji na usimamizi endelevu wa mazingira, kupambana na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwa kutii sheria za nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa mara nyengine tena kuwashukuru watendaji wote wa Tume ya Mipango kwa kazi kubwa na nzuri ya kutayarisha na hatimaye kuniwezesha kuwasilisha maendeleo haya ya hali ya uchumi na mpango wa maendeleo mbele ya Baraza lako tukufu kwa wakati. (*Makofi*)

Aidha, nawashukuru Makamishna wa Tume na Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mashirikiano na mshikamano wao. Vile vile nawashukuru Makatibu Wakuu na wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliochangia utayarishaji wa mpango huu wa maendeleo.

Shukurani za pekee ninazitoa kwa sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali kwa kushirikiana nasi katika maabara na mchakato mzima wa kukuza uchumi na maendeleo ya nchi. Mashirikiano haya ya pamoja yatatusaidia kutekeleza vyema mpango wa maendeleo. Ni matumaini yangu kuwa tutashirikiana zaidi katika matayarisho ya mpango wa maendeleo ujao.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii ya pekee kuwashukuru washirika wa maendeleo wakiwemo nchi marafiki na mashirika ya kimataifa ambao ni pamoja na ACBF, *AfDB,* AGRA, *BADEA*, BELGIUM, *CARE AUSTRIA*, CDC, CHAI, CHINA, CIDA, DANIDA, EAC, EGH, EGYPT, EU, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GERMANY, GLOBAL FUND, GRFC, DPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, OPEC, ITC, JAPAN, JICA, MCC, NORWAY, ORIO - Netherland, OMAN, KOREA, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, SWEDEN, SPAIN, UK, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, UNIDO, URT, USA, USAID, UN-HABITAT, WORLD BANK, WHO, SIPO, na WSPA.

Waheshimiwa Wajumbe, wote hawa wametoa mchango mkubwa katika maendeleo yetu na misaada yao tunaithamini na nawaomba waendelee kutusaidia katika kipindi kijacho.

Mhe. Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, naomba kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Dimani, kwa kuendelea kunisaidia na kuniamini. Nawahakikishia ushirikiano zaidi na sitawaangusha!

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili pamoja na hotuba ya Bajeti ya Serikali na hatimaye kuyapitisha mapendekezo ya mwelekeo wa uchumi kwa mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, Dkt. Mwinyihaji Makame, kwa kuwasilisha hotuba ya wizara yake inayohusu hali ya uchumi na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli zetu kwa kipindi hiki cha asubuhi zinaishia hapo na kama tunavyoelewa leo ni siku ya bajeti, ambapo shughuli hiyo itaanza saa 10:00 jioni. Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe, tuwe tayari tumefika kwa wingi, maana itakuwa sio jambo la kupendeza, tumewaalika wageni wengi na ikawa sisi wenyeji hatupo, itakuwa sio jambo la kupendeza hata kidogo.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, jioni tuwe tayari tumejaa ukumbini angalau saa kumi kasorobo iwe tayari tumeshakaa sote. Wageni waalikwa tumewaambia saa 9:30 wawe wameshakaa katika maeneo yao. Kwa hivyo, tujitahidi tufuate utaratibu huu na kwa kweli tutakuwa tunatimiza wajibu wetu ipasavyo.

Kabla sijasitisha shughuli kwa sasa, naomba nitoe taarifa ndogo sana, kwamba mara baada ya kuahirisha shughuli zetu, Waheshimiwa Wawakilishi wa upande wa CCM wabaki humu ndani. Aaaa! (*Makofi/Vicheko*)

Sijaletewa taarifa ya UKAWA. Kwa hivyo, Wajumbe wa upande wa CCM wabaki humu ndani, kuna taarifa muhimu watapewa, haitachukua muda mkubwa taarifa hiyo, lakini niendelee kusisitiza kwamba shughuli hii ya

Mpango wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo, itajadiliwa kwa pamoja kuanzia siku ya Jumatatu kama vile ambavyo Kiongozi wa Shughuli za Serikali atatoa hoja hapo baadaye kwa ajili hiyo.

Kwa hivyo, tunakubaliana kwamba tunajipanga vizuri, tutakuwa tumepata muda wa kutosha kupitia hotuba hii na vitabu ambavyo Mhe. Waziri ametuelekeza mapema, kitabu cha kwanza na cha pili. Pia na kitabu cha hotuba ya bajeti ili yote kwa pamoja yajadiliwe kuanzia siku ya Jumatatu kama itakavyoelekezwa hapo baadaye.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo, sasa nisitishe shughuli zetu hadi saa 10:00 jioni kwa ajili ya hotuba ya bajeti, ahsanteni sana.

(Saa 5:29 asubuhi kikao kiliahirishwa hadi saa 10:00 jioni)
(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe na wageni wetu mbalimbali karibuni sana, leo ni siku ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utamaduni wetu ni kwamba Waziri wa Fedha amejificha pahala sasa nawatuma *Sergeant at Arms* wakamtafute wamlete ili aje awasilishe bajeti ya Serikali. Wageni wetu tutawatambulisha baadae mara baada ya kazi ya kusoma bajeti ya Serikali, lakini kwa ujumla wageni wetu karibuni sana katika shughuli zetu za kuwasilisha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakati tunamsubiri Mhe. Waziri wa Fedha, napenda Waheshimiwa Wajumbe wakae tayari ili kuhakikisha kwamba Waziri wa Fedha tunampokea kuja kuwasilisha bajeti yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/15. *Sergeant at Arms* mtafuteni Waziri wa Fedha ili aje kuwasilisha bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Namuona sasa hivi anaingia, karibu sana Mhe. Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Wajumbe na wageni wetu wako tayari sasa kusikiliza hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar karibu Mhe. Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 Wizara ya Fedha

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kabla ya kusoma taarifa ya bajeti, naomba kutoa taarifa kwamba *paragraph No*. 9,10 na 11 zimefutwa na zisiingie katika *Hansard.*

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake tukiwemo sisi waja wake. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote uzima na uwezo wa kukutana tukiwa katika hali njema ya afya na amani ambayo inatuwezesha kujiamulia mambo yetu, yote hayo yanawezekana kwa sababu ya neema zake anazoendelea kuturuzuku neema kubwa na ndogo. Tumuombe mola wetu atuzidishie amani nchini kwetu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa faida ya nchi na wananchi wetu.

Mhe. Spika, fursa hii uliyonipa inanipa nafasi ya kutimiza matakwa ya kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata, kwa dhamira hiyo naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati maalum ya kujadili na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, mapema leo asubuhi serikali iliwasilisha mbele ya Baraza lako mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2013/14 na mwelekeo wa hali ya uchumi na mapendekezo ya mpango wa maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2014/15. Najua kwamba mazoeya yetu ni kuchanganywa kwa hotuba hizi mbili, lakini kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Wizara mbali mbali yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwezi wa Agost mwaka 2013, jukumu la usimamizi wa mipango ya maendeleo limetenganishwa na Wizara ya fedha. Naamini utaratibu huu wa kuwasilisha sekta hizi muhimu kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu na wananchi wake, unatoa fursa zaidi kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuwa na uelewa mpana zaidi wa maendeleo ya nchi, mipango yake na uwezo wake wa mapato na mgawanyo wake kimatumizi.

Mhe. Spika, nchi yetu imeshuhudia mwaka mwengine wa utulivu mkubwa, amani na maelewano mema. Pamoja na kuwa nchi yoyote haikosi matukio ya uvunjaji wa sheria, kipindi cha mwaka kinachomalizika Hotuba ya Bajeti ya Serikali, 2014/2015 tokea tulipokutana kwa wakati kama huu wa kupitia mipango yetu ya maendeleo na mapendekezo ya bajeti, kimekuwa cha kipekee ambacho imeonesha mashirikiano mazuri ya kidugu na utulivu. Wazanzibari kwa ujumla wao wamejidhihirishia wenyewe na kuwadhirihishia walimwengu kuwa wanaweza kuishi kwa amani, utulivu na mshikamano bila ya kujali tofauti za kijinsia, rangi, kabila, imani za dini na itikadi za kisiasa. Naamini hii ndio jamii ya Wazanzibari na Zanzibar tunayoitaka sote na tuna nafasi ya kuiimarisha zaidi. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuzidishie imani hii na umoja wetu, *Amin*.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba sote tumeshiriki katika kuileta hali hii ya kujivunia na kwamba wengi wetu katika jamii ni viongozi kwa namna moja au nyengine na kwa dhamana tofauti, mwenye dhamana kubwa zaidi kwa nchi yetu ni Mheshimiwa Rais wetu (Dr. Ali Mohamed Shein). Yeye ndie alietajwa na Katiba yetu kuwa Mkuu wa Zanzibar yetu. Kwa vyovyote vile, mafanikio haya tunayojivunia leo ya amani, utulivu na umoja wetu ni ishara ya uongozi wake bora, wenye uono wa mbali na unaopendelea mema kwa nchi yetu anayoiongoza na Wananchi tuliomkabidhi jukumu la kutuongoza.

Mhe. Spika, naomba basi nitumie fursa hii kutoa pongezi maalum kwa Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein (Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi) kwa kukamilisha mwaka mwengine wa fedha kwa mafanikio makubwa katika uongozi wake. Awali niligusia juu ya mabadiliko ya Muundo wa Wizara za Serikali aliyoyafanya mwezi Agosti mwaka jana, kwa nia ya kuleta ufanisi zaidi wa utendaji Serikalini. Naomba pia nitumie fursa hii adhimu kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu iliyojidhihirisha katika kunipa tena jukumu hili muhimu kwa nchi yetu, la kuiongoza Wizara ya Fedha.Natambua kuwa Wizara hii ndio moyo kwa nchi yoyote ile, hivyo naendeleza ahadi yangu kwake ya kujituma kwa nguvu, maarifa na uzoefu wangu wote ili kutimiza makusudio yake ya kunikabidhi Wizara hii.

Mhe. Spika, naelewa kwamba Kiongozi Mkuu wa nchi yetu ni mmoja tu na Urais hauna ubia, lakini naelewa pia kuwa Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya kazi kwa karibu sana na wasaidizi wake wakuu. Naamini kuwa maamuzi yote amekuwa akiyafanya baada ya kushauriana na Wasaidizi wake hao. Hivyo, wakati tukimpongeza Mheshimiwa Rais kwa mafanikio yake, naomba pia kuwapongeza sana wasaidizi wake wakuu Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad (Makamo wa kwanza wa Rais) na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi (Makamo wa Pili wa Rais); tunawashukuru wote kwa msaada na ushauri wao kwa Mheshimiwa Rais ambao umesaidia sana katika kuleta mfanikio yaliyopatikana ndani ya Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, kwaka huu 2014 Zanzibar tumeshereheka siku mbili kubwa na muhimu kwa nchi yetu. Kwanza, tumesherehekea kutimiza miaka hamsini ya Mapinduzi yetu matukufu ya tarehe 12 Januari 1964.Pili, tumesherehekea kutimia miaka hamsini ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika uliozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nichukue tena fursa hii umpongeza sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete (Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na Dr. Ali Mohamed Shein (Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi) kwa kutimiza miaka hiyo hamsini ya Muungano. Kwa Dr. Shein, tunampongeza pia kwa kutimiza miaka hamsini ya Mapinduzi yetu.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuangalia utekelezaji wetu wa mwaka wa fedha unaomalizika tarehe 30 Juni 2014, naomba nichukue fursa hii kuzungumzia mambo matatu, mawili ya msiba na moja la furaha yaliyotokea katika kipindi cha utekelezaji wa Bajeti yetu. Najua yapo mengi yaliyotokea, lakini naomba niyataje haya kwa sababu maalum.

Mhe. Spika**,** kwanza ni msiba uliolikumba Bara letu la Afrika hapo tarehe 5 Disemba 2013. Kwetu sisi binaadamu, hasa sisi waumini, tunaelewa kuwa kifo ni faradhi na kwamba hakuna nafsi ambayo haitaonja mauti, lakini bado anapoondoka miongoni mwetu na kutangulia mbele ya haki, mtu ambae ametoa mchango mkubwa sana kwa binaadam wenziwe, sote tunasikitika.

Mhe. Spika, tarehe hiyo niliyoitaja ndio alifariki mpendwa wetu, mwana wa Afrika na kioo cha utetezi wa haki Afrika na duniani kote, Marehemu Nelson Madiba Mandela. Sifa na mchango wa Mzee Mandela hasa katika kupigania haki Afrika na duniani pamoja na mchango wake katika kuleta maelewano na kustahamiliana miongoni mwa makundi yanayohasimiana, yakiwemo ya ubaguzi wa rangi ambayo yalimtesa hata yeye mwenyewe, zimeelezwa sana na sikusudii kuzirudia. Itoshe tu kuwekwa katika kumbukumbu kuwa Baraza lako tukufu nasi kwa

umoja wetu tumeungana na wananchi wa Afrika ya Kusini, wana familia ya Mzee Nelson Madiba Mandela na wapenda amani na haki duniani kote kuomboleza kuondokewa na mzee wetu, Mzee Mandela. Mungu awape moyo wa subira wanafamilia na wananchi wote wa Afrika ya Kusini.

Mhe.Spika, tukio la pili la kuhuzunisha ni la kifo cha aliyekuwa mwenzangu, mshirika wangu na kiongozi mwenzangu, marehemu William Augusta Mgimwa, aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliefariki dunia tarehe 1 Januari 2014, nchini Afrika ya Kusini alikokuwa akipatiwa matibabu. Kama nilivyotangulia kusema kuwa sisi sote ni waja wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea. Tunamuomba Mwenyezi Mungu pia ailaze roho ya marehemu William Augusta Mgimwa mahali pema, *Amin*.

Mhe. Spika, la tatu, na la furaha ni la kuteuliwa Waziri mpya wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni Waziri ambae ninamfahamu sana; kwa kuwa nimeshafanya nae kazi. Ni kijana, ni msomi, ni mchapa kazi na ni mwanamama. Kupitia Baraza lako tukufu nachukua fursa hii kumpongeza sana na kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Saada Salum Mkuya kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika wadhifa huo muhimu kwa kuitumikia Jamhuri yetu. Sina wasiwasi juu ya utendaji na mashirikiano ya Mheshimiwa Saada Salum Mkuya. Ninaamini chini ya uongozi wake, Wizara zetu mbili zitapiga hatua zaidi ya kuleta ufanisi katika utendaji na kuondoa kero chache zilizobakia.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nianze mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoendelea wa 2013/14. Hata hivyo, naomba nitangulize maneno machache juu ya matokeo ya kujivunia ya utendaji wa uchumi wetu. Najua yameshaelezwa kwa urefu asubuhi ya leo na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Ikulu na Utawala Bora, lakini na mimi naomba niyagusie kwa uchache sana ili nayo yaweze kuweka taswira bora ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti yetu kwa mwaka huo.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika mapitio ya hali ya uchumi wa Zanzibar umeonesha matumaini mazuri zaidi mwaka 2013 kwa kuzingatia kasi ya kukua kwake na utulivu wa bei za bidhaa na huduma. Uchumi umekuwa kwa asilimia 7.4 mwaka 2013 ikiwa ni kasi kubwa zaidi ya ukuaji wa uchumi kwa Zanzibar katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Mwaka 2012 uchumi ulikuwa kwa asilimia 7.1.

Mhe. Spika, kwa upande wa utulivu wa bei za bidhaa na huduma, Mfumko wa Bei umeendelea
kupungua na kufikia asilimia 5.0 kwa mwaka 2013, nao ukirekodi kiwango kidogo zaidi kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi iliyopita. Mwaka 2012 mfumko wa bei ulifikia asilimia 9.4. Kasi ndogo ya mfumko wa bei ni muhimu kwa kushajihisha uwekezaji.

Mhe. Spika, kwa upande wa muundo wa uchumi, bado hakuna mabadiliko makubwa. Sekta ya
huduma inaendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 44 ya Pato la Taifa ikifuatiwa na Kilimo asilimia 31 na Viwanda asilimia 11.3.

Mhe. Spika, Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2013/14 ilipanga kukusanya TZS 658.5 bilioni. Kati ya jumla hiyo TZS 380.6 bilioni kutoka vianzio vya ndani, ambapo *ZRB* imetarajiwa kukusanya TZS 171.7 bilioni na *TRA* kukusanya TZS 147.9 bilioni. Aidha, makadirio ya mapato kutoka kwa wafanyakazi wa *SMT* wanaoishi Zanzibar (*PAYE*) ni TZS 26 bilioni na mikopo ya ndani ni TZS 25 bilioni. Serikali pia ilitarajia kukusanya TZS 16.4 bilioni kutokana na vianzio visivyokuwa vya kodi (mapato ya mawizara) na kuuanza mwaka ikiwa na bakaa ya TZS 5 bilioni kutoka mwaka 2012/13. 23. Kwa upande wa mapato kutokana na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, jumla ya TZS 40.0 bilioni zilitarajiwa zikiwa Misaada ya Kibajeti (*GBS)* na TZS 235.4 bilioni kutokana na Ruzuku na Mikopo kutoka nje kwa ajili ya *Program* na miradi ya maendeleo.

Makadirio ya Matumizi

Mhe.Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilipanga kutumia TZS 658.5 bilioni, ambapo TZS 353.1 bilioni ni matumizi ya kazi za kawaida, TZS 70.0 bilioni kama ni mchango wa Serikali katika Miradi ya Maendeleo na TZS 235.4 bilioni mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya *Program* na Miradi ya Maendeleo. Kiasi kilichobakia cha TZS 2.5 bilioni kilipaswa kutokana na fedha za msamaha wa madeni (*MDRI*).

Matarajio Ya Mapato Na Matumizi Kwa Kipindi Cha Julai 2013-Machi 2014 (Miezi Tisa ya Bajeti)

Mapato

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2013 - Machi 2014, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya TZS 457.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, *ZRB* ilikadiriwa kukusanya TZS 121.1 bilioni, *TRA* ilikadiriwa kukusanya TZS 109.0 bilioni, mapato yasiokuwa ya kodi (Mawizara) ni *TZS* 12.2 bilioni na *PAYE* kutoka *URT* ni TZS 16.2 bilioni. Aidha, jumla ya TZS 20.0 bilioni zilitarajiwa kutokana na mikopo ya ndani na TZS 5.0 bilioni bakaa kutoka mwaka 2012/13. Misaada kutoka nje ilitarajiwa kuingiza TZS 174.3 bilioni ikiwemo TZS 27.2 bilioni za *GBS*, TZS 145.2 bilioni kwa ajili ya *Program*/Miradi ya Maendeleo na TZS 1.9 bilioni Msamaha wa Madeni.

Matumizi

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio, jumla ya TZS 409.6 bilioni zilitarajiwa kutumika ikiwemo matumizi ya kawaida ya TZS 248.7 bilioni na TZS 160.9 bilioni kwa kazi za maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida, Mishahara ilitarajiwa kugharimu TZS 119.4 bilioni, matumizi kwa Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 55.1 bilioni, Ruzuku kwa Taasisi ni TZS 34.8 bilioni na Matumizi mengineyo ni TZS 39.54 bilioni. Matumizi ya kazi za Maendeleo yalihusisha mchango wa Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo wa TZS 29.8 bilioni na misaada kutoka nje ya TZS 176.9 bilioni.

Hali Halisi Ya Mapato Kwa Kipindi Cha Julai 2013 - Machi 2014

Mhe. Spika, Mapato yote yaliyokusanywa katika kipindi cha miezi tisa yalifikia TZS 398.4 bilioni sawa na asilimia 87.0 ya matarajio ya kipindi hicho na asilimia 60.0 kwa makadirio ya mwaka.

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, mapato ya ndani yalifikia TZS 247.27 bilioni sawa na asilimia 62.1 ya mapato yote yaliyokusanywa kwa kipindi hicho. Kiwango hicho cha ukusanyaji wa Mapato kinamaanisha ukuaji wa TZS 45.8 bilioni sawa na asilimia 23 ikilinganishwa na TZS 201.5 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, kati ya mapato hayo, *TRA* imekusanya jumla ya TZS 99.3 bilioni ikiwa sawa na asilimia 91.1 ya lengo la kukusanya TZS 109.0 bilioni katika kipindi cha miezi tisa. Kiasi hicho cha ukusanyaji kinaashiria ukuaji wa mapato kwa asilimia 24.9 kutoka TZS 79.5 bilioni zilizokusanywa na *TRA* katika kipindi hama hicho mwaka uliopita.

Mhe. Spika, kati ya makusanyo ya *TRA*, Idara ya Forodha imechangia TZS 64.5 bilioni ikifikia utendaji wa asilimia 86 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho la kukusanya TZS 74.8 bilioni. Hata hivyo, kwa kulinganisha na kipindi cha miezi tisa cha mwaka 2012/13, makusanyo ya Forodha yamekuwa kwa asilimia 44 kutoka makusanyo ya TZS 44.9 bilioni yaliyopatikana kwa miezi tisa hadi Machi 2013. Kwa upande wake, Idara ya Kodi za Ndani imekusanya TZS 34.8 bilioni sawa na asilimia 97 ya lengo la miezi tisa. Utendaji huo wa Idara ya Kodi za Ndani unadhihirisha ukuaji wa mapato yake kwa asilimia 31 ikilinganishwa na TZS 26.5 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/13.

Mhe. Spika, kwa upande wa *ZRB*, makusanyo halisi hadi Machi 2014 yamefikia TZS 134.6 bilioni sawa na asilimia 110.5 ya lengo la kipindi hicho la kukusanya TZS 133.9 bilioni. Kipindi kama hicho mwaka 2012/13 *ZRB* ilikusanya TZS 109.8 bilioni. Kwa ujumla, mapato yaliyokusanywa na *ZRB* yamekuwa kwa TZS 24.8 bilioni sawa na asilimia 22.6. Mapato hayo yanahusisha pia TZS 10.6 bilioni za mapato ya mawizara ambayo mwaka jana TZS 8.8 bilioni zilikusanywa.

Mhe. Spika, Serikali pia imepokea jumla ya TZS 15.8 bilioni kutokana na Kodi ya wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar *(PAYE)*. Kiasi hicho ndicho kilichokuwa kimetarajiwa ambacho ni ongezeko la asilimia 28.5 kutoka TZS 12.3 bilioni za mwaka uliopita. Aidha, Serikali imekopa ndani *TZS* 20.0 bilioni sawa na asilimia 80 ya matarajio ya kukopa TZS 25 bilioni kwa mwaka mzima.

Mapato ya nje

Mhe. Spika, jumla ya TZS 131.1 bilioni zimepatikana kutoka nje katika kipindi cha miezi tisa ikiwa ni pamoja na TZS 27.2 bilioni za Misaada ya Kibajeti sawa na ongezeko la asilimia 32 kutoka TZS 20.5 bilioni zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/13. Hali ni tofauti kidogo kwa upande wa Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya *Program* na Miradi ya Maendeleo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio, jumla ya TZS 103.9 bilioni zimepatikana sawa na upungufu wa asilimia 47.1 ya TZS 196.3 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2012/13. Kati ya fedha zilizopatikana, Ruzuku ni TZS 32.7 bilioni na Mikopo ni TZS 71.2 bilioni. Miongoni mwa sababu za upungufu huo ni kukamilika kwa Mradi wa kuweka njia mpya ya umeme baina ya Ras Kiromoni hadi Fumba, kuchelewa kuendelea kwa mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, kuchelewa mchakato wa manunuzi kwa Mradi wa Huduma za Jamii (*ZUSP*) na matatizo ya mradi wa barabara za Pemba za Wete – Konde na Wete – Gando.

HALI HALISI YA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2013-MACHI 2014

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha miezi tisa, serikali imemudu kutumia jumla ya TZS 376.9 bilioni kwa kazi za kawaida na maendeleo, Sawa na upungufu wa TZS 51.1 bilioni ikilinganishwa na miezi tisa ya mwaka 2012/13 ambapo TZS 428.0 bilioni zilitumika. Kwa sehemu kubwa, upungufu huo umechangiwa na kushuka kwa matumizi ya kazi za maendeleo kama nilivyoeleza kabla.

Matumizi ya Kawaida

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida, serikali ilitumia jumla ya TZS 246.0 bilioni kwa miezi hii tisa (Julai 2013 - Machi 2014) sawa na asilimia 70 ya makadirio ya mwaka na asilimia 99 ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa. Sehemu kubwa ya matumizi hayo yameelekezwa katika ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi wa serikali ambayo inachukua asilimia 49 ya matumizi yote ikifuatiwa na matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali unaochukuwa asilimia 21 ya matumizi yote. Matumizi mengineyo na Ruzuku kwa Taasisi mbalimbali za serikali ni asilimia 17 na 14 ya matumizi hayo.

Mhe. Spika, kwa kulinganisha na matumizi ya TZS 205.8 bilioni yaliyofanyika kwa kazi za kawaida katika miezi tisa hadi Machi mwaka 2013, matumizi yameongezeka kwa TZS 41.8 bilioni, sawa na asilimia 19.5.

Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Mhe. Spika, jumla ya TZS 131.7 bilioni zimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo hadi kufikia Machi 2014. Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimefikia TZS 103.9 bilioni, ikiwa ni upungufu kwa asilimia 40.9 ikilinganishwa na TZS 175.8 bilioni zilotumika mwaka 2012/13. Kati ya fedha hizo za Washirika wa Maendeleo, TZS 71.2 bilioni ni Mikopo na TZS 32.7 bilioni ni Ruzuku. Upungufu huu umetokana na kuchelewa utekelezaji kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo kama nilivyoeleza awali.

Mchango wa Serikali kwa kazi za Maendeleo umefikia TZS 27.8 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 9 ikilinganishwa na mwaka 2012/13 ambapo TZS 25.9 bilioni.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, katika hatua za kuimarisha mapato kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilifanya marekebisho ya viwango vya kodi kwenye baadhi ya sheria kwa lengo la kuinua Mapato ya Serikali, kuziba mianya iliyopo na kupunguza nakisi ya Bajeti ya Serikali. Maeneo yaliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na Ushuru wa Stempu, Ada ya Uwanja wa Ndege, Ada ya Bandari, Kodi za Mafuta, Kodi za Hoteli na Leseni za Njia. Hali ya utekelezaji wa hatua hizo na matokeo yake kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, ni kama ifuatavyo:-

Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*)

Mhe. Spika, marekebisho yamefanywa katika usajili wa Hoteli kwenye *VAT* na kupunguza misamaha ya kodi. Kianzio cha *VAT* kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 kilitarajiwa kuiingizia serikali, jumla ya TZS 48.2 bilioni ambapo kianzio hicho hadi kufikia kipindi hicho kiliingizia jumla ya TZS 51.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 6.8 ya matarajio yaliyopangwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2013/14.

Kodi za Hoteli

Mhe. Spika, serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi za Hoteli Namba 1 ya mwaka 1995 katika maeneo mbalimbali ambapo hoteli zinazotoza chini ya Dola 45 ziliongezewa tozo kutoka Dola 5 hadi 8 kuanzia mwezi Septemba 2013. Kianzio hicho cha mapato kilitarajiwa kuingizia serikali jumla ya TZS 2.86 bilioni ambapo hadi kufikia kipindi cha miezi tisa kimechangia jumla ya TZS 2.67 bilioni, sawa ya asilimia 93.35.

Ushuru wa Stempu

Mhe. Spika, Serikali ililenga kushusha kiwango cha Ushuru wa Stempu kwa bidhaa muhimu za mchele na unga wa ngano na katika hati mbalimbali. Kiwango cha Ushuru wa Stempu kwa bidhaa za mchele na unga kimeshuka kutoka asilimia 3.0 hadi asilimia 2.0. Sambamba na hatua za kurekebisha Hati nyengine, hatua hiyo ilikusudiwa kuongeza jumla ya TZS 600 milioni ambapo hadi kufikia Machi 2014 jumla ya TZS 180 milioni zimekusanywa, sawa ya asilimia 30 ya matarajio.

Ada ya Uwanja wa Ndege

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu liliridhia pia kupanda kwa Ada ya Uwanja wa Ndege kutoka *USD* 35 iliyokuwa ikitumika zamani hadi *USD* 40 kwa abiria wanaosafiri kwenda nje ya Tanzania. Makusanyo ya kianzio hiki hadi Machi 2014 yamefikia TZS 1.38 bilioni, sawa na asilimia 100.1 ya Makadirio ya TZS 1.37 bilioni.

Ada ya Bandari

Mhe. Spika, Ada ya Bandari kwa abiria wanaosafiri baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ilipandishwa kutoka TZS 1,000 hadi TZS 2,000. Hatua hiyo ilikadiriwa kuingiza jumla ya TZS 1.75 bilioni. Hadi kufikia Machi 2014 jumla ya TZS 1.95 bilioni zimekusanywa, sawa na asilimia 111.4 ya makadirio ya miezi tisa.

Kodi za Mafuta

Mhe. Spika, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria za Kodi za mafuta namba 7 ya mwaka 2001 ikiwemo kuweka utaratibu wa ukusanyaji Kodi zote wakati wa uingizaji wa mafuta nchini. Utaratibu wa kubadilishana taarifa za uingiaji wa mafuta ya nishati nchini baina ya *TRA, ZRB* na Mamlaka ya Mapato ya Kenya *(KRA*) tayari umeshaanza. Mikakati hiyo iliongeza ukusanyaji wa mapato ya kodi za mafuta, ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi 2014 kulijitokeza ongezeko la jumla la TZS 3.03 bilioni ambapo matarajio ni kuongeza jumla ya TZS 5.00 bilioni ifikapo mwishoni wa Juni 2014.

Leseni ya Udereva

Mhe. Spika, Serikali ilifanya mabadiliko ya viwango vya ada ya leseni za udereva ambapo hadi mwezi Machi *ZRB* ilisajili leseni 23,924 ikiwa ni zaidi ya lengo la kusajili leseni 17,500. Viwango hivyo vipya vya ada na idadi kubwa zaidi ya leseni zilizotolewa vilipelekea makusanyo kufikia jumla ya TZS 206.89 milioni wakati makadirio ni TZS 116 milioni, sawa na asilimia 178.4 ya lengo.

Usajili wa Vyombo vya Moto

Mhe. Spika, usajili wa vyombo vya moto ulianza kutekelezwa pamoja na kubadili viwango vya ada ya usajili wa vyombo ambapo kianzio hiki kilikusanya jumla ya TZS 740 milioni kwa kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2013/14, sawa na ongezeko la asilimia 16.7 ya matarajio katika kipindi hicho ya TZS 560 milioni.

Leseni za Njia

Mhe. Spika, Serikali ilifanya mabadiliko ya utozaji wa ada za leseni za njia kwa kuongeza TZS 35 kwa kila lita ya mafuta ya Diseli na Petroli. Kutokana na utekelezaji wa hatua hiyo hadi kufikia Machi 2014 jumla ya TZS 1.8 bilioni zimekusanywa sawa na ongezeko la asilimia 12.5 ya TZS 1.6 bilioni Julai hadi Machi kwa mwaka 2012/13.

Misamaha ya Kodi

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe watakumbuka kuwa miongoni mwa hatua zilizoahidiwa na serikali katika kuongeza mapato ni kudhibiti zaidi misamaha ya kodi na kupunguza kiwango cha kusamehewa kodi. Hatua hii imeleta matunda mazuri kwani kwa ujumla, misamaha ya Kodi imeshuka kutoka TZS 30.7 bilioni zilizosamehewa hadi Machi 2013 sawa na asilimia 38.6 ya mapato ya *TRA* yaliyokadiriwa katika kipindi hicho hadi TZS 14.9 bilioni sawa na asilimia 15 ya mapato ya *TRA* yaliyokadiriwa hadi Machi 2014. Mafanikio hayo yamechangia katika ukuaji wa asilimia 44 wa mapato ya Forodha kama nilivyoeleza awali.

Deni la Taifa

Mhe. Spika, mpaka kufikia mwezi wa Machi 2014, Deni la Taifa limeongezeka hadi kufikia TZS 294.90 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 17.0 ikilinganishwa na deni la TZS 252.3 bilioni lililokuwepo mwezi wa Machi 2013. Ukuaji huu umetokana na kutolewa fedha kwa ajili ya Miradi inayoendelea kama vile ya ujenzi wa njia ya kujitayarishia ndege kuruka *(Taxiway*) na maegesho ya ndege *(Apron)*, miradi ya maji safi na salama na miradi ya barabara.

Kati ya deni hilo, TZS 211.8 bilioni ni Deni la Nje linalomaanisha ongezeko la asilimia 4.0 ikilinganishwa na TZS 203.8 bilioni kwa mwezi wa Machi 2013. Asilimia 88 ya deni la nje linadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na asilimia 12 ilidhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). *(Makofi)*

Mhe. Spika, hadi mwezi wa Machi 2014 deni la ndani nalo liliongezeka hadi kufikia TZS 83.09 bilioni ikilinganishwa na TZS 48.5 bilioni kwa mwezi wa Machi 2013, sawa na ongezeko la asilimia 71.3. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa mikopo kupitia Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*), deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na deni la Wastaafu (viinua mgongo).

MWELEKEO WA BAJETI 2014/15

Malengo Makuu ya Serikali

Mhe. Spika, Bajeti ya Serikali itaendelea kuongozwa na dhamira ya serikali ya kuimarisha mapato yake ya ndani, kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma. Kutokana na kasi ya asilimia 2.8 ya ukuaji wa idadi ya watu Zanzibar kama ilivyobainishwa na Sensa ya Idadi ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012, nchi yetu kwa sasa inakadiriwa kuwa na watu 1,339,000. Utafiti wa Hali ya Jamii na Uchumi wa mwaka 2013 unaonesha kuwa kati ya idadi hiyo, tuna watoto 230,377 katika Skuli za Msingi na watoto 70,677 katika Skuli za Sekondari za Serikali.

Mhe. Spika, kwa upande wa huduma za afya, tuna vituo vya afya na Hospitali vinavyofikia 144 hapa nchini ambavyo kwa jumla vimehudumiwa wagonjwa 298,226 mwaka jana. Huduma zote hizi ni muhimu kwa ustawi wa wananchi na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, bajeti itaendelea kujikita katika malengo makuu ya kujenga jamii yenye siha, iliyoelimika kwa elimu bora na inayoimarika kiuchumi. Utekelezaji wa malengo hayo unaendana na malengo ya Dira ya 2020.

Maeneo ya Kipaumbele

Mhe. Spika, Mpango wetu wa Maendeleo umeainisha maeneo ya kipaumbele, miongoni mwake ni haya yafuatayo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii;
ii. Kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo elimu bora, huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama;
iii. Kuimarisha huduma kwa makundi maalum hususan wazee wasiojiweza, watoto na watu wenye ulemavu;
iv. Kuimarisha mazingira ya biashara kwa kuondoa vikwazo visivyo vya lazima na urasimu;
v. Kuiendeleza Sekta binafsi hususan katika uzalishaji na utoaji wa huduma muhimu kupitia ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*);
vi. Kuharakisha upatikanaji wa ajira bora hasa kwa vijana; na
vii. Kuimarisha utafiti ili kuwezesha mipango bora.

MAANDALIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU (*PBB*)

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana, serikali imeendelea na matayarisho ya kutumia utaratibu wa bajeti inayotumia Programu. Tayari Wizara zote zimemudu kuandaa Programu hizo katika mwaka unaoendelea wa fedha. Lengo la utaratibu huo mpya ni kuongeza msisitizo wa kupata matokeo yanayohitajiwa kutokana na matumizi ya fedha za umma, uwazi na uwajibikaji zaidi katika matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, kwa ajili ya kikao hiki cha bajeti, Wizara zote zimetayarisha bajeti kwa Mfumo wa Programu na mfumo uliozoeleka wa vifungu, lengo ni kuwapa Waheshimiwa Wawakilishi uelewa wa awali wa namna bajeti itakavyokuwa inawasilishwa chini ya Mfumo wa *PBB*. Ingawa kwa mwaka huu bado uidhinishaji wa bajeti utatumia mfumo uliozoeleka, Waheshimiwa Wajumbe wana fursa ya kuangalia na kuchangia kupitia bajeti ya *PBB*. Mafunzo kamili ya mfumo huo wa *PBB* yatatolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe katika mwaka ujao wa fedha.

MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2014/15

Mapato

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 707.8 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 7.5 ya makadirio ya mwaka 2013/14 ya TZS 658.5 bilioni. Hata hivyo, makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 28.0 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya TZS 552.9 bilioni yanayotarajiwa kukusanywa hadi kufikia Juni 2014.

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, jumla ya TZS 365.8 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kama mapato ya ndani katika mwaka 2014/15. Ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya TZS 326.0 bilioni hadi kufikia mwaka 2014, ukuaji huo ni sawa na asilimia 12.2 ya makusanyo halisi yanayotarajiwa kwa mwaka 2013/14. Kati ya makadirio ya 2014/15, *ZRB* inakadiriwa kukusanya jumla ya TZS 199.7 bilioni yakiwemo na makusanyo ya Mawizara ya TZS 18.4 bilioni. Makadirio hayo yanaashiria ukuaji wa asilimia 20.0 ya Matarajio ya mwaka 2013/14 ya TZS 172.5 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande wake, *TRA* inakadiriwa kukusanya TZS 166.1 bilioni sawa na ziada ya asilimia 25.7 ya mapato halisi yanayotarajiwa kwa mwaka 2013/14 ya *TZS* 132.1 bilioni.

Aidha, mapato yanayotokana na wafanyakazi wa *SMT* wanaofanya kazi Zanzibar yanakadiriwa kufikia shiling 21.0 bilioni kwa mwaka 2014/15 sawa na matarajio yake kwa kipindi cha Julai hadi Juni 2013/14. Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15 inatarajia kukopa ndani jumla ya shiling 15.0 bilioni ili kufidia nakisi ya bajeti.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato ya nje serikali kwa mwaka 2014/15 inakadiria kukusanya jumla ya shiling 305.4 bilioni ikiwa ni ongezeko la shiling 78.5 bilioni sawa na asilimia 30.0 ya matarajio ya makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai hadi Juni mwaka 2014 ya shiling 226.9 bilioni.

Kati ya mapato hayo, shiling 265.4 bilioni ni Mikopo na Ruzuku kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho ni ongezeko la shiling 82.5 bilioni sawa na asilimia 45.1 ikilinganishwa na matarajio ya kipindi cha Julai hadi Juni 2014 ya shiling 182.9 bilioni (ikiwemo matarajio ya msamaha wa madeni wa TZS 1.9). Kiasi kilichobakia cha shiling 40.0 bilioni ni msaada wa kibajeti sawa na matarajio ya kipindi cha Julai hadi Juni 2014.

Matumizi

Mhe. Spika, Serikali inakadiria kutumia jumla ya shiling 707.8 bilioni mwaka 2014/15, sawa na ziada ya asilimia 7.5 ya makadirio ikilinganishwa na shiling 658.5 bilioni kwa mwaka 2013/14. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mapato, ikilinganishwa na matumizi halisi ya shiling 552.9 bilioni yanayotarajiwa hadi Juni 2014, ongezeko halisi ni asilimia 28.0.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Mhe. Spika, matumizi ya kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia jumla ya shiling 376.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 15.5 ya matarajio ya mwaka 2013/14 ya shiling 326.0 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Mishahara ya Serikalini TZS 184.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia12.4. ya matarajio hadi Juni 2014 ya shiling 164.1 bilioni;
ii. Ruzuku kwa Taasisi za Serikali shiling 50.3 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 7.2 ya matarajio hadi Juni 2014;
iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali shiling 69.8 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 23.3 ya matarajio ya mwaka 2013/14 ya TZS 56.6 bilioni; na
iv. Matumizi mengineyo yakuendeshea serikali ni shiling 71.8 bilioni kwa sawa na ongezeko la asilimia 22.9 ya matarajio ya mwaka 2013/14 ya TZS 58.4 bilioni.

Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa awali wakati wakuwasilisha Mpango wa Maendeleo, Serikali inatarajia kutumia jumla ya shiling 331.3 bilioni mwaka 2014/15 kugharamia utekelezaji wa mpango huo, ikilinganishwa na matumizi halisi ya shiling 226.9 bilioni yanayotarajiwa hadi mwisho wa mwezi Juni 2014, kunajitokeza ongezeko la shiling 104.4 bilioni sawa na asilimia 46.0. Kati ya matumizi hayo, shiling 265.4 bilioni ni misaada kutoka nje, ikiwemo shiling 66.3 bilioni za ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shiling 199.1 bilioni ni Mikopo. Ikilinganishwa na shiling 182.9 bilioni zinazotarajiwa kutumika hadi Juni 2014, kunajitokeza ongezeko la TZS 82.5 bilioni, sawa na asilimia 45.1 ya matumizi halisi yanayotarajiwa hadi Juni 2014.

Mhe. Spika, kwa upande wa mchango wa serikali, kiasi cha shiling 65.9 bilioni zinatarajiwa kutumika ikiwa ni ongezeko la shiling 21.9 bilioni, sawa na asilimia 49.7 kutoka matumizi halisi ya shiling 44.0 bilioni yanayotarajiwa kufanywa hadi kumalizika mwaka wa 2013/14. Katika matumizi ya mwaka 2014/15, mkazo utaelekezwa katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo miundombinu, maji safi na salama, umeme, elimu na afya.

Mhe. Spika, kiasi cha shiling 267.1 bilioni kinakusudiwa kutumika katika maeneo ya vipaumbele sawa na asilimia 80.7 ya bajeti yote ya Kazi za Maendeleo. Mchanganuo wa matumizi hayo ya maeneo ya kipaumbele ni kama hivi ifuatavyo:-

i. Miundombinu (uwanja wa ndege na barabara) shiling 160.1 bilioni sawa na asilimia 48.4 ya bajeti yote ya maendeleo. Kiasi hicho cha mtumizi kinatokana na kuanza tena utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kufuatia kukamilika kwa mazungumzo baina ya Serikali na Mkandarasi juu ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza;
ii. Afya imetengewa shiling 30.6 bilioni sawa na asilimia 9.3 ya makadirio ya matumizi ya kazi za Maendeleo;
iii. Elimu imetengewa shiling 28.4 bilioni sawa na asilimia 8.6 ya bajeti ya kazi za maendeleo;
iv. Maji safi na salama iliyotengewa shiling 26.8 bilioni sawa na asilimia 8.1;
v. Ujenzi wa meli mpya ya abiria uliotengewa shiling 20 bilioni sawa na asilimia 6.1 ili kukamilisha meli hiyo inayotarajiwa kukamilika mwezi Februari mwakani na kuwasili nchini mwezi Aprili; na
vi. Upelekaji umeme kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vya Makoongwe na Kisiwa Panza, Pemba unaotarajiwa kugharimu shiling 1.2 bilioni. Lengo ni kutimiza ahadi ya serikali ya kuwafikishia umeme wananchi wenzetu wanaoishi katika visiwa hivyo.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie maeneo mengine matatu muhimu ambayo yanagusa sana maisha ya wananchi wetu.

Eneo la kwanza, ni suala la mishahara ya wafanyakazi wa utumishi wa umma. Serikali iliahidi kuimarisha maslahi ya wafanyakazi wake kila hali ya uchumi na mapato ya serikali inaporuhusu. Ili kutekeleza azma hiyo, katika kipindi cha miaka minne hii ya awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi, tayari mapitio makubwa ya mishahara ya wafanyakazi yamefanyika mara mbili.

Kwanza Oktoba mwaka 2011 kwa kuzingatia zaidi maslahi ya wataalamu kwa nia ya kuwabakisha nchini wataalamu wetu baada ya kuhitimu masomo yao.

Nyongeza ya pili ilifanyika mwezi Oktoba mwaka 2013 kwa kuzingatia zaidi wafanyakazi wa muda mrefu na wenye uzoefu.

Mhe. Spika, mishahara imeendelea kuchukua sehemu kubwa ya mapato yetu ya ndani na matumizi ya kazi za kawaida. Kwa mwaka ujao wa fedha, mishahara ya Serikali na Taasisi zake zinazopokea ruzuku inatarajiwa kufikia asilimia 55.2 ya matumizi yote ya kazi za kawaida.

Kwa kuwa mishahara ni miongoni mwa malipo ya lazima na ya kwanza kulipwa, inabidi kuendelea na zoezi la kuimarisha maslahi kwa hadhari ili lisikwamishe shughuli nyengine za utendaji wa serikali na kazi za maendeleo. Kwa kuzingatia hali hiyo, serikali haikusudii kuongeza mishahara kwa mwaka ujao wa fedha, badala yake itaendelea kufanya marekebisho kwa wafanyakazi ambao hawakupata marekebisho ya nyongeza walizostahili na kuendelea kutoa nyongeza za mwaka.

Mhe. Spika, eneo la pili ni suala la ruzuku kwa pembejeo za kilimo. Suala la ruzuku limekuwa na malumbano katika sehemu nyingi duniani. Kwetu sisi hili ni suala muhimu kwa kusaidia kuimarisha ukulima na wakulima wetu hususan kwa kuzingatia mkakati wetu wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Serikali itaendelea kushuhudia matokeo mazuri ya kilimo hasa cha mpunga yakichangiwa, miongoni mwa sababu nyengine ni uamuzi wetu wa kutoa ruzuku kwa pembejeo za kilimo.

Takwimu zinaonesha kuwa uzalishaji wa mpunga umefikia Tani 33,655 mwaka 2013 ambacho ndicho kiasi kikubwa zaidi kuvunwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Serikali itaendelea na utaratibu huo wakutoa ruzuku kwa pembejeo za kilimo katika mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, eneo la tatu ni elimu. Itakumbukwa kuwa tokea Mapinduzi matukufu, Sera ya Serikali imekuwa ni kutoa elimu bila ya malipo kwa wananchi wote, Unguja na Pemba. Sera hii imekuwa chachu kubwa yakuwawezesha na kuwakomboa watoto wetu, wakiwemo wanyonge, kujipatia elimu kwa ngazi zote. Pamoja na kwamba kumekuwa na utaratibu wa wazazi kuchangia kwa mambo madogo madogo, kimsingi serikali imeendelea kutoa elimu bila ya

malipo. Kwa mnasaba wakutekeleza dhamira ya sera ya elimu bila ya malipo. Kwa mwaka ujao wa fedha serikali inafuta malipo yanayofanywa na wazazi kwa ajili ya mitihani ya Kidato cha Sita *(A-Level).* Badala yake, kama ilivyo kwa mitihani ya Kidato cha nne *(O-Level),* Serikali italipia gharama zote za mitihani hiyo.

HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO 2014/15

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, serikali haikusudii kuongeza kodi katika vianzio vyake vya mapato zaidi ya kuimarisha usimamizi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, badala yake, ni Ada ya Usalama wa Anga pekee ambayo inapendekezwa kuongezwa kwa madhumuni yakuimarisha uwezo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(ZAA).*

Mhe. Spika, kwa upande wa hatua za kiutawala, maeneo yanayotarajiwa kusimamiwa kwa karibu ni pamoja na haya yafuatayo:

i. Kuimarisha usimamizi wa kimaeneo *(Block Management System)* na kuwatambua walipakodi zaidi ili waingizwe katika wigo wa kodi. Zoezi hili litashirikisha *ZRB, TRA,* Msajili wa Kampuni na Biashara, Baraza la Manispaa na Halmashauri za Wilaya;
ii. Kuzitambua na kuzichukulia hatua nyumba zote zinazotumiwa kulaza wageni *(villas)* bila ya kuwa na usajili. Lengo ni kuhami mapato ya serikali na kuepusha kutumika vibaya nyumba hizo ili kunusuru usalama wa nchi, wananchi na wageni wetu;
iii. Kuhusisha utaratibu wa zuio katika Ushuru wa Stempu kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika Kodi ya Ongezeko la Thamani. Lengo ni kuwaingiza katika wigo wa kodi wafanyabiashara wanaotoa huduma za usambazaji wa huduma mbalimbali katika Sekta ya Utalii;
iv. Kuimarisha zaidi ukaguzi wa walipakodi katika sekta maalum kama vile za mawasiliano, utalii na mafuta ya petrol; na
v. Kuimarisha matumizi ya Teknohama na usimamizi *(Supervision*) katika *ZRB* na *TRA*.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa awali, katika mchakato wa kuandaa bajeti kwa mwaka ujao wa fedha, serikali pia ilishirikiana na wadau mbalimbali katika kuangalia kwa kina changamoto zinazoikabili Sekta ya Utalii, Mazingira ya Kibiashara na Uimarishaji wa mapato nchini. Kazi hii ilifanyika chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Tume ya Mipango kwa utaratibu wa Maabara. Matokeo ya kazi hiyo ni mapendekezo kadhaa ambayo tayari serikali imeyaridhia kwautekelezaji katika mwaka ujao wa fedha, 2014/15.

Mhe. Spika, kwa upande wa Ukusanyaji wa mapato, hatua zilizopendekezwa ni hizi zifuatazo:-

Mapato yasiyo ya Kodi

Gawio kutoka Mashirika ya Serikali

Mhe. Spika, Serikali inamiliki Mashirika yanayoendeshwa kibiashara. Matarajio ni kuwa siyo tu Mashirika hayo yaweze kutoa huduma zilizokusudiwa kwa kuanzishwa kwake, pia yaweze kuchangia katika bajeti ya serikali kwa kutoa gawio kutokana na faida wanayoipata.

Kuanzia mwaka ujao wa fedha, serikali itaongeza kiwango cha gawio kutoka asilimia 10 ya faida kwa sasa hadi asilimia 20. Haitarajiwi kuwa utaratibu huu utaathiri utendaji wa mashirika kwani bado yatabakishiwa asilimia 80 ya faida itakayopatikana. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato kwa shiling 630 milioni.

Kupunguza Kiwango cha Ushuru wa Mirathi

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikichukua jitihada maalum za kusajili ardhi na majengo yaliopo nchini. Kwa upande wa mali za serikali, zoezi hili litasaidia serikali kujua kwa uhakika mali zake zote. Kwa mali za watu binafsi, zoezi hili linatarajiwa kusaidia sana kupunguza matatizo yakugombania ardhi, kupunguza umaskini kwa kuruhusu mali hizo kutumika katika kupata mikopo ili iweze kuimarisha shughuli za kiuchumi na kupunguza matatizo ya kijamii hasa katika mirathi.

Mhe. Spika, hata hivyo, imebainika kuwa kwa sasa, moja ya kikwazo kinachotajwa sana kuzuia usajili huo wa mali ni kiwango cha asilimia 5 cha Ushuru wa Mirathi. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, serikali inakusudia kupunguza kiwango hicho hadi asilimia 0.25. Kiwango hicho kinatarajiwa kuruhusu watu wenye uwezo mdogo nao kusajili mali zao na kukamilisha matakwa ya mirathi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya serikali kwa shiling 750 milioni kwa mwaka 2014/15.

Kufanya Mapitio ya Viwango vya Ada mbalimbali Serikalini

Mhe. Spika, katika kutoa huduma zake, serikali imekuwa ikitoza ada mbalimbali. Imebainika kuwa bado vingi ya viwango vya ada hizo ni vya zamani sana na vimepitwa na wakati. Serikali inakusudia kuvifanyia mapitio viwango hivyo katika mwaka ujao wa fedha angalau viendane na wakati, bila ya kuathiri utoaji wa huduma hizo.

Mapato ya Kodi

Mashine za Risiti

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuuziwa bidhaa mbalimbali bila ya kupatiwa risiti zinazostahiki. Hali hii pia inaathiri mapato ya serikali na hivyo uwezo wake wa kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Kwa upande mwengine, utoaji wa risiti umeendelea kuwa wa kizamani na usiokwenda na wakati. Kwa mwaka ujao wa fedha, serikali inakusudia kuanzisha utaratibu wa kutolewa risiti kwa kutumia mashine maalumu pia zenye fursa ya kusaidia ukusanyaji wa mapato *(Electronic Fiscal Devices – EFDs).* Utaratibu huo utakuwa ni sehemu ya kufanya biashara nchini kuwa ya kisasa zaidi na utasimamiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Utaratibu huu unatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali kwa shiling 5,600 milioni mwaka 2014/15.

Utaratibu Maalum kwa Walipakodi wadogo

Mhe. Spika, katika hotuba yangu kwa mwaka unaoendelea wa fedha niliomba na serikali kuridhia na hatimae Baraza la Wawakilishi kuidhinisha kuanzishwa kwa utaratibu maalum *(Presumptive Tax System)* wa utozaji kodi kwa Wafanyabiashara wadogo ambao mauzo yao hayapindukii shiling milioni 10 kwa mwaka. Hata hivyo, utaratibu huu haukuweza kutekelezwa kutokana na masuala ya kiutendaji. Kwa mwaka ujao, utaratibu huo unakusudia kuanza rasmi chini ya usimamizi wa *ZRB* badala ya *TRA* iliyokubaliwa awali. Kiasi cha shiling 900 milioni zinatarajiwa kukusanywa kupitia utaratibu huo.

Kuanzisha Msimamizi wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu

Mhe. Spika, kutokana na kuimarika kwa uwekezaji na biashara nchini, kumejitokeza pia biashara ya huduma mbalimbali zinazohitajika katika uwekezaji huo, ikiwemo huduma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu. Kampuni kadhaa zimeanzishwa na tayari zinatoa huduma hizo sambamba na ushauri wa masuala ya kodi. Kwa bahati mbaya, hadi sasa hakuna chombo kinachosimamia (*Regulater)* fani hiyo hapa Zanzibar. Badala yake, tumeendelea kutumia viwango vya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi ya Tanzania Bara *(NBAA)* na viwango vya Kimataifa.Serikali inakusudia kuondosha kasoro hiyo kwa kuanzisha rasmi Msimamizi huyo. Inatarajiwa kwamba hatua hiyo itasaidia katika kuongeza Mapato ya Serikali kwa shiling 450 milioni.

Kuimarisha Utathmini wa Forodha

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo linaangaliwa na serikali kwa hatua za kiutawala ni uimarishaji wa uthamini wa bidhaa zinazoingia nchini *(valuation)* katika Idara ya Forodha ya *TRA*. Pamoja na juhudi zilizochukuliwa, bado wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakiikosesha mapato Serikali kwa kufanya udanganyifu ukiwemo wakushusha thamani halisi ya bidhaa zao. Hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa zinatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali kwa shiling 2,500 milioni katika mwaka ujao wa fedha.

Kupunguza Misamaha ya Kodi

Mhe. Spika, mwaka jana serikali ilichukua hatua maalum yakupunguza misamaha ya kodi na kubakia na ile tu, ama ya lazima kwa kuvutia uwekezaji maalum au ni muhimu kwa mashirikiano yetu na nchi nyengine au ufadhili wa

miradi ya umma. Serikali ilipunguza msamaha wa kodi kutoka asilimia 100 kwa vifaa vya uwekezaji na kubakisha asilimia 80. Kwa utaratibu huo, muwekezaji anaeingiza vifaa vya uwekezaji nchini alilazimika kulipa kiasi cha asilimia 20 ya kodi za uingizaji na kusamehewa kiasi kilichobakia cha asilimia 80. Kwa mwaka ujao wa fedha, inapendekezwa kupunguza zaidi kiwango cha kusamehewa na kuwa asilimia 75 tu kama ilivyo Tanzania Bara. Wawekezaji watalazimika kulipa kiasi kisichosamehewa cha asilimia 25 ya kodi.

Mhe. Spika, kwa ujumla, hatua zote zilizopendekezwa katika maabara zinatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali kwa shiling 10.4 bilioni katika mwaka 2014/15.

Marekebisho ya Sheria

Mhe. Spika, ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, inapendekezwa kubadilisha baadhi ya sheria kama ifuatavyo:-

Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ya mwaka 199**8**

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na matatizo ya utozaji kodi kwa Kampuni za simu za mikononi baina ya pande mbili za Muungano. Msingi wa kutozea kodi ni pahali huduma ilipotolewa. Kwa sasa, Kampuni moja tu ya mawasiliano ina makao makuu yake Zanzibar wakati nyengine tatu zina makao makuu Tanzania Bara. Tatizo ni kuwa Kampuni hizo zimekuwa zikiwasilisha marejesho yake katika upande wenye makao makuu bila ya kujali huduma imetolewa wapi. Matokeo yake ni matatizo yanayopelekea kushtakiana Mahakamani kuhusiana na malipo ya *VAT* hususan juu ya kodi ya manunuzi *(Input Tax).*

Mhe. Spika, kwa dhamira ya kutatua tatizo hilo *TRA* na *ZRB* zimefanya vikao na kukubaliana namna bora yakushughulikia. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kurekebisha Kanuni chini ya Sheria ya *VAT*. Baada ya marekebisho hayo, *TRA* na *ZRB* zitakusanya mapato kutegemea vigezo vya uwiano wa matumizi (*voice and non-voice traffic mails*), majumuisho ya muda wa maongezi, vocha na huduma nyengine na kuruhusu kodi za manunuzi kuwasilishwa *TRA* na *ZRB*. Kutakuwa na fomula maalum ya kugawana mapato ya mauzo ya Kampuni za Simu kila mwezi.

Sheria ya Usimamizi wa Kodi namba 7 ya mwaka 2009

Mhe. Spika, utaratibu wa sasa ni kwa mlipakodi kubaki na mapato aliyokusanya mwezi mmoja hadi siku ishirini na tano (25) katika mwezi unaofuata.Utaratibu huu una kasoro ya kuchelewesha mapato hayo kuingia serikalini na hivyo kuathiri uwezo wake wa kutoa huduma na kuiingiza katika gharama.Ili kuondoa kasoro hiyo, inapendekezewa kubadilisha muda wa kuwasilisha Ritani kutoka siku kumi na tano (15) baada ya kumalizika mwezi na kuwa siku saba (7) na muda wa kulipa kodi kuwa siku kumi na nne (14) baada ya kumalizika mwezi badala ya siku 25 za sasa.

Sheria ya Ada za Bandari namba 2 ya mwaka 1999

Mhe. Spika, ili kuimarisha uwezo wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kutoa huduma bora zaidi, inapendekezwa kuongeza Ada ya Usalama wa Anga kwa wasafiri wa ndani tu kutoka Shiling 1,000 ya sasa hadi Shiling 3,000. Nyongeza hii haihusishi wasafiri wa nje ya nchi ili kutoathiri utalii. Kiwango hicho pia kitawiana na kiwango ambacho tayari kinatumika Tanzania Bara.

Sheria ya Usafiri Barabarani Namba 7 ya mwaka 2003

Mhe. Spika, Zanzibar bado ina utaratibu wa kutoa upya leseni za udereva kila mwaka (*renew*) na nyengine kwa kipindi cha hadi miaka mitatu. Utaratibu huu umeonekana kuleta usumbufu kwa madereva kwa kuhitajika kurudi *ZRB* kila mwaka na wakati mwengine kwa msongamano. Kwa nia ya kupunguza tatizo hilo, inapendekezwa kuongeza muda wa kuhitaji kupata tena leseni. Leseni ambayo kwa sasa inatolewa kwa mwaka mmoja itatolewa kwa miaka miwili ya miaka miwili iwe mitatu na leseni ya miaka mitatu iwe miaka mitano.

Mhe. Spika, **s**ambamba na mabadiliko hayo, inapendekezwa pia kuvifanyia mapitio vifungu vya Ada za Leseni ili viendane na utaratibu huo mpya. Viwango vipya vinavyopendekezwa ni Shiling 35,000.00 kwa leseni ya miaka miwili, Shiling 45,000.00 kwa leseni ya miaka mitatu na Shiling 60,000.00 kwa leseni ya miaka mitano.

SURA YA BAJETI

Mhe. Spika, kwa ujumla, serikali inatarajiwa kutumia jumla ya shiling 707.8 bilioni kwa mwaka wa fedha 2014/15, kati yake matumizi ya kawaida ni shiling 376.5 bilioni na kiasi kilichobakia cha Shiling 331.3 bilioni kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kati ya matumizi ya Shiling 707.8 bilioni, shiling 306.0 bilioni zinatarajiwa kutokana na mchango wa Washirika wa Maendeleo zikiwemo Shiling 265.4 bilioni kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo, shiling 40.0 bilioni kwa ajili ya misaada ya kibajeti (*GBS*) pamoja na shiling 0.6 bilioni kutokana na fedha za msamaha wa madeni.

Mhe. Spika, ukiondoa mapato hayo ya misaada, serikali inahitaji jumla ya shiling 401.8 bilioni kutokana na mapato yake ya ndani. Kati ya kiasi hicho, shiling 365.8 bilioni zinatarajiwa kutokana na vianzio vya ndani vya kodi na visivyo vya kodi. Kwa kuzingatia matarajio ya kukusanya jumla ya shiling 323.2 bilioni hadi mwisho wa Juni 2014, kiwango hicho kinamaanisha matarajio ya ukuaji wa mapato kwa shiling 42.6 bilioni sawa na asilimia 13.1 ya makusanyo halisi yanayotarajiwa kwa mwaka 2013/14. Ukuaji huo unatarajiwa kutokana na kuimarisha utendaji wa taasisi za kodi (Shiling 32.2 bilioni) na hatua zilizopendekezwa na maabara ya ukuzaji mapato (Shiling 10.4 bilioni).

Mhe. Spika, hali hiyo bado itaacha nakisi ya shiling 36.0 bilioni katika Bajeti ya Serikali. Kodi kutokana na wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar (*PAYE*) inatarajiwa kufikia shiling 21.0 bilioni itasaidia kupunguza nakisi hio hadi shiling 15.0 bilioni. Inapendekezwa kukopa ndani ya nchi kiasi hicho cha shiling 15.0 bilioni ili kuziba pengo hilo na hivyo kuleta uwiano wa bajeti (Mapato na Matumizi).

Jadweli namba 1 linaonesha kwa muhtasari mchanganuo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Jadweli Namba 1: Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2014/2015

Maelezo	Makisio 2013/14 (TZS Bil.)	Makisio 2014/15 (TZS Bil.)	Ongezeko (%)
MAPATO			
A Mapato ya ndani	324.6	365.8	*12.7*
B 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	40	40	*0*
C Dhamana za Hazina na Hati Fungani	25	15	*-40*
D Kodi ya Mapato kwa W/Kazi wa SMT	26	21	*-19.2*
E Bakaa ya Bajeti 2013/14	5	0	*-100*
F Msamaha wa Madeni (MDRI)	2.5	0.6	*-76*
G Mikopo na Ruzuku	235.4	265.4	*12.8*
Jumla ya Mapato	**658.5**	**707.8**	*7.5*
MATUMIZI			
Matumizi ya Kawaida	**353.1**	**376.5**	***6.6***
i) Mishahara (Mawizara)	155.5	184.5	*18.7*
ii) Mishahara (Ruzuku)	20.8	23.7	*13.6*
iii) Matumizi Mengineyo (Wizara)	80.6	71.8	*-10.9*
iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku)	31.2	26.7	*-14.6*
v) Mfuko mkuu wa Serikali (CFS)	65	69.8	*7.4*
Matumizi ya Maendeleo	**305.4**	**331.3**	*8.5*
i) Mchango wa Serikali	70	65.9	*-5.9*
ii) Washirika wa Maendeleo	235.4	265.4	*12.8*
Jumla ya matumizi	**658.5**	**707.8**	**7.5**

Chanzo: Wizara ya Fedha

Mhe. Spika, pamoja na juhudi za kuimarisha mapato, serikali itaendeleza jitihada zake za kudhibiti matumizi ili fedha za umma zielekezwe katika maeneo yenye tija zaidi. Watendaji wote wenye dhamana ya matumizi watasisitizwa kuwa na muamko zaidi wa kuthamini na kusimamia fedha za umma. Serikali inakusudia kuandaa utaratibu wa kupunguza matumizi yote yanayoepukika yakiwemo ya kutumia washauri wa nje katika maeneo ambayo uwezo wa utaalamu wa ndani upo, semina hasa zinazofanyika katika hoteli za kitalii wakati kumbi za kufanyia semina hizo zimo ndani ya taasisi zetu na safari zisizo za lazima. Wote tunahitaji kuhakikisha kuwa tunapata mafanikio makubwa zaidi kwa fedha kidogo tulizonazo. Serikali bado italifanyia kazi suala la semina ambazo zingepaswa kugharamiwa na serikali.

SHUKRANI

Mhe. Spika, tumekuwa tukikutana na kujadiliana na hatimaye kuamua mambo yetu kupitia ndani ya Baraza lako tukufu kwa amani na umoja. Pamoja na ukali wa mijadala badhi ya nyakati, bado tumeweza kuikhitimisha kwa makubaliano na hivyo kujenga heshima ya chombo chetu hiki muhimu. Mafanikio haya hayakuja tu yenyewe, bali yanatokana na umahiri wa Uongozi wa Baraza hili unaoanzia kwako wewe Mhe. Spika. Naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi na wasaidizi wako wote kwa kuendesha kwa ufanisi mkubwa shughuli za Baraza hili.

Mhe. Spika, kupitia kwako naomba pia kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza lako na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa mashauriano, miongozo na mashirikiano ya hali ya juu wanayotupatia. Shukurani zangu maalum kwako ni kwa michango yao katika mchakato wa maandalizi ya bajeti hii ninayoiwasilisha leo.

Mhe. Spika, natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu na wafanyakazi wa wizara mbalimbali, idara zinazojitegemea, Mikoa, Wilaya, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Asasi zisizo za Kiserikali pamoja na Sekta Binafsi kwa mchango wao katika kufanikisha ukamilishaji wa Bajeti hii na nyaraka nyengine zinazoambatana nazo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natoa shukurani maalumu kwa wasaidizi wangu wakuu katika Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu, ndugu Juma Ameir Hafidh, Kamishna na watendaji wote wa Idara ya Bajeti, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Idara ya Fedha za Nje na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha na hatimae leo hii kuiwasilisha hotuba hii. Aidha, nashukuru pia mchango wa Bi. Amina Khamis Shaaban, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na watendaji wake kwa mashirikiano ya karibu yaliyosaidia kurahisisha kazi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maendeleo yetu tunayoyashuhudia yanaendelea kupata nguvu kutokana na mchango wa nchi rafiki na mashirika ya kimataifa. Kwa mnasaba huo na kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar. Naomba kuthamini na kushukuru sana msaada wa Canada, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, China, Japan, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki.

Mhe. Spika, natoa pia shukrani kwa Mashirika ya Kimataifa yafuatayo kwa misaada yake ya mali na ufundi kwa Zanzibar. Mashirika yenyewe ni: *ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank* ya *China, EXIM Bank* ya *Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-ABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, World Bank, WHO* na *WSPA. (Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Spika, mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa bajeti yetu unaonesha kuwa tunapiga hatua katika maendeleo yetu, lakini bado tuna kazi kubwa ya kuharakisha maendeleo hayo. Kwa mwaka 2014/15 kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita, bado tumekabiliwa na kazi kubwa sana mbele yetu ya kuimarisha uchumi, huduma za jamii na wigo na ukusanyaji wa mapato kutokana na vianzio vyetu vya ndani. Tunahitaji kuendeleza umoja wetu na kujituma zaidi ili lengo la kujiletea maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla liweze kufikiwa. Hii si kazi

rahisi, lakini kwa jitihada za pamoja inawezekana. Ni matumaini yangu kuwa sote tutashirikiana zaidi katika mwaka ujao wa fedha ili tutimize azma yetu muhimu ya kupiga hatua za haraka katika kutekeleza maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima na taadhima naliomba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimaye kwa kauli moja liidhinishe Makadirio ya Mapato ya shiling mia saba na saba bilioni na mia nane milioni na matumizi ya kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kugharamia kazi za kawaida ya shiling 376.5 bilioni na Mpango wa Maendeleo kwa shiling 331.3 bilioni kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Asante sana, Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Bajeti ya Serikali na kutumia muda kiasi saa moja na dakika saba, hoja ambayo Waheshimiwa Wajumbe mmeiunga mkono na kwamba mko tayari ijadiliwe wakati muwafaka.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hotuba hiyo ya Bajeti ya Serikali kama nilivyoahidi kabla katika mkutano huu au kikao hiki, tumewaalika wageni mbalimbali ambapo wengi wao nashukuru wamefika. Kwa hiyo, naomba sasa niwatambue wageni wetu ambao wako pale juu ukumbini. *(Makofi)*

Kwanza napenda kutambua kuwepo kwa Mhe. Mama Asha Suleiman, najua makofi hayo ni kwa sababu Mama Asha Suleiman ana kawaida mikutano yote au vikao vyote vya bajeti huwa anakuja. Nitambue kuwepo vilevile kwa Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi. Napenda tutambue kuwepo kwa Kiongozi, Mabalozi wadogo waliopo Zanzibar, Balozi mdogo wa Misri, naomba asimame. Vilevile naomba nitambue Mabalozi wengine wadogo waliopo Zanzibar, naomba kwa pamoja wasimame. Naomba pia tutambue kuwepo kwa Wawakilishi wa Mabalozi waliopo hapa Zanzibar, *Representatives of the Council General Based in Zanzibar, please*. *(Makofi)*

Vilevile, naomba tutambue kuwepo kwa Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa yaliopo Zanzibar, *Representatives of the UN welcome,* karibuni sana. Naomba tutambue kuwepo kwa Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tutambue pia kuwepo kwa Makamanda mbalimbali wa Brigedia Nyuki, pamoja na Idara Maalum ziliopo hapa Zanzibar kwa pamoja naomba wasimame. Pia, yupo katika waalikwa Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar. Naomba niwakaribishe na kuwatambua ndugu zetu Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali ziliopo Zanzibar. Pia, yupo Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania namuomba asimame, inaonekana hakufika. Waalikwa wengine ni Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali pia nao tumewaalika nawaomba wasimame. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa naye pia yupo katika ukumbi huu namuomba asimame. Nawaomba tuwatambue wawakilishi wa vyama mbalimbali vya siasa nao pia tumewaalika nategemea wapo hapa, nawaomba wasimame. Tumewaalika vilevile Makamishna wote kutoka wizara mbalimbali nawaomba wasimame, tumewaalika Wenyeviti wa Tume mbalimbali ziliopo Zanzibar, nawaomba wasimame, hawapo? Nawaomba wasimame Wakurugenzi wa wizara na idara mbalimbali ambao tumewaalika na kama wapo nawaomba wasimame. *(Makofi)*

Kuna wageni maalum wanafamilia wa Spika, nawaomba nao sasa wasimame. Tumewaalika Waandishi wa Habari mbalimbali, nawaomba nao wasimame kwa ujumla wao, wageni hao wanaongozwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, kama yupo namuomba asimame, amedharurika. Waheshimiwa Wajumbe, naomba mkubali na muwakaribishe sana wageni wetu hao mbalimbali. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa watulivu wakati wa kusikiliza hotuba hii ya bajeti na kuna tangazo moja muhimu sana ambalo Mhe. Waziri wa Bahari, Utamaduni na Michezo ameniomba nitangaze kwenu.

Mhe. Waziri wa Bahari, Utamaduni na Michezo anatoa taarifa kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba ili kuwapa nafasi nzuri ya kuitafakari vizuri Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na ubalozi mdogo wa Misri hapa Zanzibar imewaandalia Waheshimiwa burudani maalum ya kikundi cha Utamaduni kutoka Misri. Burudani hiyo itafanyika siku ya Ijumaa tarehe 16/5/2014 kuanzia saa 2: 30 katika ukumbi wa Studio wa Rahaleo. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Habari anawaondolea wasiwasi kwa sababu burdani hii itahudhuriwa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wake zao na pia Waheshimiwa Wajumbe pamoja na waume zao na kwa wale ambao Waheshimiwa Wajumbe wana mke zaidi ya mmoja wasiwe na wasiwasi utaratibu Mheshimiwa anauandaa kwa ajili ya hiyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mnakaribishwa sana na kadi za mualiko zitapatikana hapa Barazani kesho. Kwa hiyo, mkija hapa mtapokea kadi za mualiko huo kwa ajili ya burudani hiyo itakayofanyika katika ukumbi hapo Rahaleo.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo na kwa mujibu wa Kanuni ya 93(5), naomba nimkaribishe kiongozi wa shughuli za serikali ndani ya Baraza hili ambae kwa niaba yake amkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais ili atoe hoja ya kuakhirisha shughuli zetu hizi mpaka siku za Jumatatu ili Waheshimiwa Wajumbe wapate kutafakari na kusoma kwa karibu sana Bajeti ya Serikali pamoja na mpango wa serikali. Mhe. Waziri wa Nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizo mbele yetu zimemalizika kwa Mhe. Waziri wa Fedha kuwasilisha rasmi Bajeti ya Serikali na kwa kuwa muda wetu bado upo na kwa sababu ya Kanuni, naomba Mhe. Spika, Baraza lako tukufu hili tuweke Kanuni ya muda kando ili tuweze kuakhirisha shughuli zetu kwa leo na turudie tena siku ya Jumatatu tarehe 19/5/2014 saa 3:00 za asubuhi barabara.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na wageni wetu mara baada ya kuakhirisha kikao hichi, tunawakaribisha wote Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni tukutane pale nje ili tuweze kubadilishana maelezo kidogo na wakati huo huo kupata viburudishaji vilivyotayarishwa kwa ajili ya shughuli ya leo ya kikao cha Bajeti ya Serikali. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hichi hadi siku ya Jumatatu tarehe 19/5/2014 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 11:26 jioni Baraza liliakhirishwa hadi siku ya Jumatatu
tarehe 19/5/2014 saa 3:00 asubuhi)